# KUCHUNGUZA DHIMA ZA NYIMBO ZA NGOMA YA MSONDO WA PEMBA

**ASHA RASHID MOHD**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI MASHARTI YA KUPATIA SHAHADA YA UZAMILI (M.A: KISWAHILI FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2015**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu yenye mada: ***"Kuchunguza Dhima za Nyimbo za Ngoma ya Msondo wa Pembe",*** na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa kwa ajili ya Utahini wa shahada ya Uzamili ya Chuo kikuu huria cha Tanzania.

é é é é é é é é é é ..é é é é é .

Professa Tigiti S. Y. Sengo

(Msimamizi)

é é é é é é é é é é é é é é

Tarehe

## HAKI MILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile Tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile Kieletroniki, Kurudufu Nakala Kurekodi au njia yoyote nyingine Bila ya idhini ya Mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa Niaba.

# TAMKO

Mimi **Asha Rashid Mohd,** nathibitisha kuwa hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyengine yoyote

é é é é é é é é é é é é é

Saini

é é é é é é é é é é é é é é é

Tarehe

# TABARUKU

Tasnifu hii ni zawadi mahsusi kwa wazee na jamaa zangu, walimu wangu tokea shule za Msingi hadi kufikia Vyuo Vikuu popote walipo.

## SHUKURANI

Kwanza kabisa ninamshukuru Allah (S.W) Mwingi wa Rehema, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo, kwa kunijaalia uhai, uzima, afya njema na uwezo wa kwenda huku na kule hadi nikakamilisha kazi hii, yote ni kudra na kadari Yake. Sina budi, pia kutoa shukurani zangu za dhati, kwa msimamizi wangu, Professa Sheikh Tigiti S.Y.M. Sengo, kwa kunisimamia na kunipa mwngozo hadi kukamilika kwa kazi hii. Bila ya juhudi yake njema na usimamizi imara nisingaliweza kufanikiwa. Kadhalika, ninamshukuru mwalimu Bakari Kombo Bakari wa OUT-Pemba, kwa kutuongoza, kutushajihisha na kutuhimiza hadi kukamilika tasnifu zetu.

Shukurani nyengine ni kwa wazazi wangu, bwana Rashid Mohammed Rashid na bibi Arafa Mpemba, kwa kunipa nasaha na kunilelea watoto wangu wakati nilipokuwa masomoni. Shukurani za dhati ni kwa mume wangu mpenzi bwana Feisal Abdalla Said, kwa kunisaidia kwa hali na mali, na kunipa utulivu wakati wote wa kuitayarisha na kuifanya kazi hii. Shukurani nyengine ni kwa wale wote walionisaidia katika kufanikisha utafiti huu. Miongoni mwao ni:

Sheha wa Shehia ya Kengeja, Sheha wa Shehia ya Mwambe, Sheha wa Mkungu kwa kuniruhusu kuingia katika viambo vyao na kuwahoji wananchi wenzao, bibi Tijara wa Kidishi- Kengeja, bibi Asha Massoud wa Mjiweni, bibi Hadia Matano wa Mahduthi, bibi Mpaji Kibwana wa Mahduthi, bwana Khamis Suleiman wa Mahduth, bibi Hadia Buga wa Chaleni- Mwambe. Mwalimu mkuu wa Shule ya Sekndari ya Kengeja pamoja na walimu wote kwa kunipunguzia mzigo wa vipindi wakati wote wakutayarisha tasnifu hii.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu kuchunguza dhima za nyimbo za ngoma ya msondo. Utafiti ulifanyika katika shehia ya Kengeja, Mwambe na Mkungu- Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini- Pemba. Lengo kuu la utafiti huu ni kukusanya, kuchunguza na kuzianisha dhima za nyimbo za ngoma ya msondo [wa kike]. Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni nadharia ya Uamilifu, nadharia ya Simiotiki (Uashiriji), na nadharia ya Sosholojia (Ujamii). Data zilikusanywa kutoka uwandani kwa kutumia mbinu ya usaili na mbinu ya kushirki. Aidha njia ya maktabani ilitumika kwa kusomwa tasnifu tafauti, vitabu na majarida. Matokeo ya utafiti ni dhima zilizopatikana ni dhima ya kuelimisha kwa kuonya, kufunza, na kuhimiza maadili mazuri katika maisha ya ndoa. Aidha, dhima ya kuburudisha maharusi imejitokeza katika nyimbo za ngoma ya msondo. Mafunzo ya nyimbo hizi ambayo yamejitokeza ni ustahamilivu wa shida na matatizo katika ndoa, kumuenzi na kumdhibiti mume au mke, kuwapenda na kuwathamini wakwe, kutunza usafi na kujipamba mke mbele ya mume wake, kuwacha tabia mbaya, kumuheshimu na kumtii mume. Kwa upande wa vipengele vya fani vilivyosaidia kufikisha mafunzo kwa walengwa ni lugha ya ishara, taswira, tashhisi, tauria, tashbiha, kejeli, na kadhalika kama vinavyojitokeza katika uchambuzi wa vipengele hivyo katika sura ya nne.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ..... ii

**HAKI MILIKI** ..... iii

**TAMKO LA MTAHINIWA** ..... iv

**TABARUKU** ..... v

**SHUKURANI** ..... vi

**IKISIRI** ..... vii

**ORODHA YA VIAMBATANISHI** ..... xii

**ORODHA YA VIFUPISHO** ..... xiii

**SURA YA KWANZA** ..... 1

**UTANGULIZI WA JUMLA** ..... 1

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ..... 1

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti ..... 4

1.4 Madhumuni ya Utafiti ..... 6

1.5 Madhumuni Mahsusi ..... 6

1.6 Maswali ya Utafiti ..... 6

1.7 Umuhimu wa Utafiti ..... 7

1.7.1 Kwa Wasomaji wa Fasihi ..... 7

1.7.2 Kwa Jamii ..... 7

1.7.3 Kwa Matumizi ya Nadharia ..... 8

1.8 Vikwazo vya Utafiti ..... 8

1.9 Utatuzi wa Vikwazo vya Utafiti ..... 8

1.10 Sababu za Kuchagua Mada............................................................................ 8
1.11 Hitimisho .......................................................................................................... 9
**SURA YA PILI ........................................................................................................ 10**
**UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ......... 10**
2.1 Utangulizi ....................................................................................................... 10
2.2 Maana ya Utalii................................................................................................ 10
2.3 Maana ya Kazi Tangulizi.................................................................................. 10
2.4 Maana ya Nyimbo ........................................................................................... 10
2.5 Aina za Nyimbo ............................................................................................... 11
2.6 Dhima za Nyimbo ........................................................................................... 12
2.7 Mkabala wa Kinadharia.................................................................................... 16
2.7.1 Nadharia ya Uamilifu .................................................................................... 17
2.7.2 Nadharia ya Simiotiki..................................................................................... 17
2.7.3 Nadharia ya Sosholojia................................................................................... 18
2.8 Sababu za Kuteua Nadharia.............................................................................. 19
**SURA YA TATU.................................................................................................... 20**
**MBINU ZA UTAFITI............................................................................................ 20**
3.1 Utangulizi wa sura............................................................................................ 20
3.2 Mbinu za Kukusanya Data................................................................................ 20
3.2.1 Mbinu ya Usaili............................................................................................... 21
3.2.2 Mbinu ya Kushiriki ........................................................................................ 22
3.2.3 Mbinu ya Maktabani ...................................................................................... 22
3.2.4 Kundi Lengwa.................................................................................................. 23
3.2.2 Uteuzi wa Watafitiwa....................................................................................... 23

3.4 Eneo la Utafiti ........................................................................ 24

3.5 Maadili ya Utafiti ........................................................................ 24

3.6 Mipaka ya Utafiti ........................................................................ 25

3.7 Vifaa vya Utafiti ........................................................................ 25

3.8 Hitimisho ........................................................................ 26

**SURA YA NNE ........................................................................ 27**

**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ........................................ 27**

4.1 Utangulizi ........................................................................ 27

4.2 Uwasilishaji wa Data ........................................................................ 27

4.3 Uchambuzi wa Data ........................................................................ 31

4.3.1 Dhima ya Kuelimisha ........................................................................ 31

4.3.2 Dhima ya Kuonya ........................................................................ 47

4.3.3 Dhima ya Kuburudisha ........................................................................ 56

4.4 Mafunzo Yanayopatikana Katika Nyimbo za Ngoma ya Msondo ........................................................................ 57

4.4.1 Mafunzo ya Ustahamilivu wa Shida na Matatizo Yanayotokea Katika Maisha ya Ndoa ........................................................................ 57

4.4.2 Mafunzo ya Kumuheshimu na Kumuenzi Mume au Mke ......................... 60

4.4.3 Mafunzo ya Kumuenzi na Kumdhibiti Mume au Mke ............................. 63

4.4.4 Mafunzo ya Utunzaji wa Siri za Maisha ya Ndoa ................................... 67

4.4.5 Mafunzo ya Kuwapenda na Kuwathamini Wakwe na Jamaa wa Mume au Mke ........................................................................ 71

4.4.6 Mafunzo ya Kuwacha Tabia Mbaya ........................................................ 74

4.4.8 Mafunzo ya Kujenga Mashirikiano na Maelewano Katika

Maisha ya Ndoa ........................................................................................ 76

**SURA YA TANO ........................................................................................ 83**

**HITIMISHI, MUHTSARI NA MAPENDEKEZO ............................................ 83**

5.1 Utangulizi ........................................................................................ 83

5.2 Hitimishi ........................................................................................ 83

5.3 Muhtasari wa Utafiti ........................................................................................ 84

5.3.1 Matokeo ya Utafiti ........................................................................................ 84

5.4 Mapendekezo ya Utafiti ........................................................................................ 86

**MAREJELEO ........................................................................................ 89**

**VIAMBATANISHI ........................................................................................ 93**

## ORODHA YA VIAMBATANISHI

Kiambatanishi Na. I: Maswali ya Mahojiano Yaliyotumika Katika Kukusanya Data ........................................................................... 93

Kiambatanishi Na. II: Nyimbo za Ngoma ya Msondo Zilizotumika Katika Utafiti 95

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibar |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| S. W | Subhana Wataala |
| S. A. W | Swalaahu ALaihi Wasalamu |
| USA | United State of America |
| OUT | The Open University of Tanzania |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti kaonyesha usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, madhumuni mahsusi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti, utatuzi wa vikwazo vya utafiti na sababu za kuchagua mada hii ya utafiti.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

ôNyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimuziki. Wimbo ni utungo wa shairi au utungo mfupi ulioundwa kwa maneno ya kipekee yenye muziki na yanayoleta mvuto katika kuimbwa au uimbajiò (Wamitila 2003).

Msokile (1981), anaeleza kuwa, nyimbo ni mawazo yanayoimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalum. Waimbaji huimba baada ya kupata mguso fulani wa ndani ya jamii. Matteru (1987), amesema, ñNyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi ya melodi, mapigo na muwala. Nyimbo huweza kuimbwa ni mtu mmoja pekee yake au na wenzake wakiitikia. Nyimbo ni lazima, izingatie lugha ya kisanii na iwe inaeleza maisha ya watu katika jamii.

ñKichanga kilipobahatika kutoka tumboni mwa mama yake kilitangaza shukurani zake kwa wimbo ulioitwa sauti ya kilio. Kila alipohisi njaa, woga, khofu na kadhalika, alitoa sauti ya kutaka huduma. Mama yake alielewa fasili hiyo ya

kichanga chakeò (Sengo 2009). Sengo (2009), anaeleza kwamba, halipo la kupitiwa na wakati, hakuna fikira au mawazo potofu. Dunia haiendi ila kwa uhalisia wa juzi, leo na kesho, kwa mtazamo huo, wa uhalisia, hatuna budi kuelewa kuwa kizuri cha leo kina mizizi ya kizuri cha juzi, hivyo, nia ni kutaka kurudi na kuelewa umuhimu wa Fasihi simulizi ili kurudisha maadili yetu yaliyopoteaò.

Kwa mujibu wa bibi Tiyara wa Sokoni Kengeja, Ngoma ya msondo, ilianza kabla ya uhuru. Ngoma hii ilishirikisha wanawake tu kwa lengo la kuwafundisha wari juu ya maisha yao ya baadaye (maisha ya ndowa). Ngoma hii, asili yake ilikuwa inachezwa ndani tu chini ya kiongozi wake aliyejulikana kwa jina la Nyakanga na waliopewa mafunzo hayo waliitwa wari. Ngoma hiyo huwa na jumla ya ngoma tatu zinazojuilikana kwa majina ya tutu, mchapuo na msondo na ndiyo sababu ya kuitwa ngoma ya msondo. Ngoma hiyo, baadaye ilipigwa nnje siku za sherehe za harusi na ikaongezewa ngoma nyengine inayoitwa zumari. Hapo sasa ikawa ngoma hiyo siyo ya wanawake peke yao, na wanaume walishiriki kwa kiasi kidogo tu. Ama kwa miaka mitano au zaidi, ngoma hiyo imekuwa adimu, hii ni kutokana na watu kuiga mila na dasturi za kigeni.

Ngoma ya msondo, ambayo ni taasisi yenye mchango mkubwa wa kutoa mafunzo kwa watarajiwa wa ndoa, nyimbo zake huwa na mafunzo mengi, juu ya maisha ya kijamii na kiutamaduni. Mafunzo hayo huwasaidia maharusi katika maisha yao ya ndoa msisitizo ni kuwa wastahamilivu na kuwekeana heshima na kuthaminiana, kwani, babu na bibi zetu waliishi, wakazaa na kujukuu wakiwa pamoja kutokana na kuwa wastahamilivu na kwa kuyatumia mafunzo waliyopewa na wazazi na walezi wao, walikuwa na mapenzi ya kweli, jambo ambalo leo hii limekosekana katika ndoa

zetu na ndio sababu ya ndoa zetu kuvunjika bila matarajio. Nyimbo za ngoma ya msondo ni miongoni mwa taasisi inayotumika katika kutoa mafunzo kwa wanandoa na kwa jamii kwa jumla. Ngoma ya msondo mara nyingi hupigwa katika sherehe za harusi, huweza kupigwa ndani au nje, wanawake ndio wahusika wakuu katika ngoma hii wakiwa na lengo la kutoa mafunzo kwa maharusi. Mafunzo hayo huwasaidia wanajamii katika maisha yao ya ndoa, kwa kuishi kwa furaha na kuweza kuidumisha ndoa yao. Mafunzo hayo ni msingi mkuu wa maisha ya ndoa. Ndoa kama kiini cha maisha ya familia, hulazimika zienziwe ili ziweze kuimarika na kudumishwa siku hadi siku. Uimara wa ndoa, ndiyo tegemeo la kuimarika kwa familia, ingawaje mke kwa upande wake ndiye anayezingatiwa zaidi katika uimarishaji huo kuliko mume, ndiyo maana, nyimbo nyingi za ngoma ya msondo huimbiwa zaidi mwanamke kuliko mwanamume. Hata maandalizi ya kumuenzi na kumshughulikia mume hufanywa zaidi kwa mwanamke.

Kwa mujibu wa Bi Hadia Buga wa Chaleni Mwambe, katika kuwaandaa wanandoa watarajiwa, zamani, enzi za mababu na mabibi zetu kulikuwa na taasisi za jando na unyago, ambazo zilitoa mafunzo juu ya maisha ya utuuzima yakiwa ni pamoja na maisha ya ndoa. Hayo yaliwezesha kudumu kwa ndoa nyingi, hadi kufikia kufa mmoja wapo au kutengana kwa sababu za msingi, kama vile, ukatili, ufuska, utovu wa misingi ya wazi ya Dini. Hali hiyo ni tafauti na ya leo. Kila siku tunashuhudia ndoa na talaka za ghafla ambazo hazifuati taratibu za Dini na hatima yake, ndoa hizo hazidumu

Historiya inatueleza kwamba, zamani katika jamii za Wapemba, kulikuwa na taasisi za jando na unyago ambazo zilikuwa zikifanya kazi nyumbani na maporini. Lengo la

taasisi hizo lilikuwa ni kuwaandaa vijana katika maisha ya utuzima ikiwa na pamoja na maisha ya ndoa. Hali hiyo iliwafanya vijana wahitimu, wakifikia kuwa pamoja, waweze kuishi, katika hali ya kuvumiliana, hadi mmojawapo alipofariki dunia au kutokea sababu za msingi, ndipo itokee talaka. Katika kipindi hiki cha UGENI MWINGI, jamii zetu zimeiga mila na dasturi za kigeni ambazo huendeshea shughuli za harusi zao kinyume kabisa na misingi ya Kiafrika. Mfano wa sherehe hizo ni ñHina Partyò na Kitchen Partyò. Sherehe hizo hazitoi mafunzo yoyote kwa wanandoa bali ni ufakhari wa kujionesha tu na ukusanyaji wa vyombo na pesa kwa hila.

Kutokana na hali hiyo, mtafiti amevutika kufanya utafiti huu, ili kuisaidia jamii, iweze kurudia mila na dasturi za asili,, kama vile, sherehe za jando na unyago, ngoma zinazokubalika, kwa mfano ngoma hii ya msondo wa kike, ambayo hutoa mafunzo kwa wari wanapotaka kuolewa. Aidha kutaka kuisaidia jamii, kuishauri kuwachana na mila na dasturi za kigeni ambazo haziendani na mila na dasturi za jamii zetu, na badala yake jamii zirudie mila na dasturi zetu ambazo zimewachwa kwasababu ya kutaka kwenda na wakati. Mtafiti amekusudia kuchunguza na kuzianisha dhima zinazopatikana kwenye nyimbo za ngoma ya msondo wa kike, kwani mada hii haijafanyiwa utafiti katika kiwango cha Uzamili. Mtafiti amelipata tatizo hili katika jamii kwa kuona namna zinavyoendeshwa shughuli za harusi ambapo ni kinyume na mila na dasturi za Wapemba, pia kwa kusoma utafiti mwingi wa kabla na kuliona pengo hili la utafiti.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Tatizo la utafiti ni kuachwa kwa matumizi ya nyimbo za msondo wa kike kumesababisha utovu wa maadili katika ndoa, hali ambayo imesababisha ongezeko

la wajane kutokana na kufanyika ndoa za haraka haraka na talaka za papo kwa papo. Hali hiyo, imewatia wanawake wengi, kuishi maisha ya upweke, unyonge, maradhi, na ya kukata tamaa. Tatizo hili linatokana na kuwachwa kwa mila na dasturi za jamii na kufuata tamaduni ambazo hazilingani na mila na dasturi za jamii zetu.

Mtafiti baada ya kusoma tasnifu za watu tafauti zinazohusiana na mada ya utafiti huu, amebaini waandishi kama, Sengo (1985), amechunguza mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za msanja wa Makunduchi. Katika utafiti huo aliona kuwa, nyimbo za msanja wa Makunduchi hutoa mafunzo juu ya malezi kwa vijana na pia hutoa mafunzo juu ya maadili mazuri yanayomsaidia mwanajamii kujua namna ya kuishi kulingana na jamii yake. Raya (2002), yeye amechunguza nyimbo za harusi za wanawake Waswahili wa Mombasa, katika utafiti wake yeye alijikita zaidi na mitindo kutokana na fonolojia, sintaksia, msamiati, semantiki na lugha iliyotumika.

Haji (2005) na Saada (2007), wao wamechunguza mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za harusi katika ndoa za Unguja. Katika tasnifu zao waligundua kuwa, nyimbo hizo hutoa mafunzo kwa wanandoa katika kujenga, kuimarisha na kudumisha uhusiano, mapenzi na udugu katika ndoa yao. Mdungi (2010), alichunguza nafasi ya mafumbo katika nyimbo za harusi. Katika utafiti wake aligundua kuwa, nyimbo za harusi hutumia mafumbo ambayo ndiyo yanayoibua mafunzo kwa maharusi na kwa jamii kwa ujumla, akitaja mafumbo hayo alitaja tamathali za usemi kama vile sitiari, tashbiha, tash-hisi, ishara na taswira. Naye Silau (2013), katika utafiti wake amechunguza dhima za nyimbo za Kikaguru katika kukuza na kuimarisha malezi kwa jamii ya Kikaguru. Ndumbaro (H.T), alichunguza

dhima na dhamira katika nyimbo za kabila la Wamatumbi. Akifafanua dhamira za nyimbo hizo alieleza kuwa nyimbo za Wamatumbi zina dhamira ya maadili mema, dhamira ya umoja na mshikamano nakadhalika, dhima alizozigundua ni dhima ya kuelimisha na dhima ya kuburudisha. Mtafiti wa kazi hii alichunguza dhima za nyimbo za ngoma ya msondo wa Pemba ilikuziba pengo la utafiti lililoachwa na watafiti wengine.

## 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni kukusanya, kuchunguza, kuchambua na kuzianisha dhima za nyimbo za ngoma ya msondo wa Pemba.

## 1.5 Madhumuni Mahsusi

1.5.1 Kukusanya nyimbo za ngoma ya msondo

1.5.2 Kuchunguza na kuziainisha dhima zinazopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo.

1.5.3 Kuchambua mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo.

1.5.4 Kujadili vipengele vya fani vilivyosaidia kufikisha mafunzo kwa walengwa.

## 1.6 Maswali ya Utafiti

1.6.1 Je, ni zipi nyimbo za ngoma ya msondo?

1.6.2 Je, ni dhima gani zinazopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo?

1.6.3 Je, ni mafunzo gani yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo?

1.6.4 Je, ni vipengele gani vya fani vilivyosaidia kufikisha mafunzo kwa walengwa?

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

### 1.7.1 Kwa Wasomaji wa Fasihi

Utafiti huu, utasaidia kuhifadhi nyimbo za ngoma ya msondo wa kike ambazo zinaonekana kutoweka kwa kasi kubwa kutokana na kuwachwa kwa ngoma ya msondo kwa mbadala wa kuiga kinyaninyani, ada za kigeni zilizoingizwa kwa jina la maendeleo, usasa kumbe ni ugeni, kama kwamba, Uswahilini hakukuwa na elimu ya Ulimbe na Utunduizi. Jamii, ikisharudishwa kwenye fahamu za elimu zao, nyigenyige za kinyani zitakoma na maisha yataanza upya kwa misingi ya Wapemba wenyewe.

Utafiti huu pia, utawasaidia wataalamu wa fasihi, Maprofessa, wahadhiri, walimu na wanafunzi kupata data muhimu zinazohusu nyimbo za ngoma ya msondo. Aidha, watafiti watakaohitaji kufanya utafiti katika uwanja huu wa nyimbo za msondo wa Pemba watapata taarifa za kuanzia. Utafiti huu utasaidia walimu na wanafunzi kupata marejeleo mapya ya somo lao la fasihi simulizi.

### 1.7.2 Kwa Jamii

Utafiti huu pia utazinduwa waliozugwa na kasumba za Ugeni kwa jina la usasa na utandawizi. Kila jamii iishi kwa yake, kwa misingi yake, jadi na tamaduni zake, mila na dasturi zake, lugha na fasihi zake, dhanna na fahamu za jamii ya watu wake. Aidha, utafiti huu, utasaidia kuamsha ari na kuzizindua taasisi za kijamii kuanza upya na kutathmini mila na dasturi za asili za jamii za Kipemba. Utafiti pia utasaidia kuzinduwa waliozungwa na kasumba za Ugeni kwa jina la usasa na utandawizi. Kila jamii iishi kwa yake, kwa misingi yake, jadi na tamaduni zake, mila na dasturi zake, lugha na fsihi zake, dhanna na fahamu za jamii ya watu wake.

### 1.7.3 Kwa Matumizi ya Nadharia

Utafiti huu utasaidia kutanua maarifa na kuongeza ujuzi juu ya matumizi ya nadharia, hii ni kutokana na ufafanuzi wa nadharia tafauti zilizojadiliwa na kutumiwa.

## 1.8 Vikwazo vya Utafiti

Nyimbo za ngoma ya msondo wa Wapemba hazijaandikiwa sana, kwa hivyo mtafiti alipata shida kupata kazi tangulizi kwa wingi katika maktaba. Aidha, mtafiti alipata mashaka kuwapata watafitiwa wake kutokana na shughuli zao za kimaisha kulingana na mazingira yao. Mtafiti alilazimika kwenda usiku ili ashiriki katika ngoma kwa kupata data zaidi.

## 1.9 Utatuzi wa Vikwazo vya Utafiti

Mtafiti alilazimika kusoma kazi tangulizi maktaba, makavazi na kwenye mitandao mbalimbali. Aidha, mtafiti alilazimika kuwafuata watafitiwa wake wakati wowote aliopangiwa`na watafitiwa wake, na pia mtafiti alishiriki katika shughuli ambayo ilipigwa ngoma ya msondo makusudi kwa mtafitiwa kuzidi kuona kwa vitendo.

## 1.10 Sababu za Kuchagua Mada

Nyimbo za ngoma ya msondo ni miongoni mwa taasisi kongwe zilizotumika kutoa mafunzo kwa vijana juu ya maisha yao na mbinu za kutumia katika kukabiliana na maisha hayo katika jamii, lakini leo nyimbo hizo hazitumiki tena kwa kisingizio cha usasa. Kwa hivyo, mtafiti amechagua mada hii ili kuizindua jamii ili kuzirudisha mila na dasturi za jamii na kuondosha mawazo potofu juu ya mila na dasturi za kale, kwani wahenga husema ñvya kale ni dhahabuò

### 1.11 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti kaeleza usuli wa mada, tamko la tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, madhumuni mahsusi ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti, utatuzi wa vikwazo na sababu za kuchagua mada ya utafiti.

# SURA YA PILI

# UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, dhanna tafauti zinazohusu mada zimejadiliwa, kama vile maana ya nadharia, maana ya kazi tangulizi, maana ya nyimbo nakadhalika. Nadharia zilizojadiliwa ni nadharia ya Uamilifu, nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Sosholojia. Aidha, mtafiti amezungumzia kazi tangulizi alizopitia na jnsi alivyofaidika nazo, kazi tangulizi kuhusu nyimbo kwa ujumla na nyimbo za harusi ilikubaini yaliyofanywa kwenye tafiti nyengine ambayo yaliyomsaidia kwa namna fulani katika utafiti huu.

## 2.2 Maana ya Utalii

Utalii ni namna ya usomaji kwa lengo la kupekuwa taaluma iliyojificha. Kwa kulielewa hili, mtafiti alilazimika kusoma, vitabu, majarida, tasnifu za watafiti waliomtangulia, mitandao, ili kufichuwa siri za watafiti watagulizi na kupata maarifa zaidi na wepesi wa kufanya utafiti huu.

## 2.3 Maana ya Kazi Tangulizi

Kazi Tangulizi ni jumla ya utafiti uliyofanyika, ambao unalingana na mada ya utafiti husika. Omari (2001), Kazi tangulizi hutoa ujuzi na maarifa ya wanazuoni waliowahi kufanya kazi yenye mwelekeo na lengo la mtafiti. Pia kazi tangulizi, humsaidia mtafiti kutambua mambo yepi yamefanyiwa utafiti na yapi bado.

## 2.4 Maana ya Nyimbo

Nyimbo ni dhanna yenye maana pana ambayo imeelezwa na wataalamu tafauti, kati ya hao ni: TUKI (2004), wameeleza kuwa, nyimbo ni tungo za kishairi zenye

kutumia mahadhi ya melodi, mapigo na muwala. Nyimbo huweza kuimbwa ni mtu mmoja pekee au na wenzake, wakiitikia. Nyimbo ni lazima, izingatie lugha ya kisanii na iwe inaeleza maisha ya watu katika jamii.

Msokile (1981), amesema, nyimbo ni mawazo yanayoimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalumu. Waimbaji huimba baada ya kupata mguso fulani wa ndani ya jamii. Matteru (1987), ameeleza kuwa nyimbo za ngoma (Mwelema) ni aina ya nyimbo za ngoma zinazoimbwa kwa lengo la kufurahisha katika mikutano au sherehe. Nyimbo hizi huimbwa wakati wa kucheza ngoma.

Wamitila (2003), ameeleza, nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizo huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimuziki. Wimbo ni utungo wa shairi au utungo mfupi ulioundwa kwa maneno yenye muziki na yanayoleta mvuto katika kuimbwa au uimbaji. Kwa mtazamo wa mtafiti, nyimbo ni utanzu wa ushairi ambao huwa na mpangilio wa maneno na uimbaji ambao hutoa ujumbe kwa hadhira iliyohusika.

## 2.5 Aina za Nyimbo

Mulokozi (1989), amezitaja aina za nyimbo, ni pamoja na nyimbo za kidini, nyimbo za vita, nyimbo za taifa, nyimbo za kuwinda, nyimbo za watoto, nyimbo za jandoni (Nyiso), nyimbo za kubembeleza watoto (Bembea), nyimbo za harusi (Tumbuizo), nyimbo za kuaga mwaka (Kongozi), nyimbo za kilimo (Wawe), nyimbo za kilio (Mbolezi), na nyimbo za baharini (Kimai). Mtafiti amegundua kuwa, ziko na nyimbo

za ngoma, kwa mfano, nyimbo za ngoma ya msondo, ambazo ni nyimbo za kuwafunza maharusi ili kuweza kukabiliana na maisha mapya ya ndoa.

## 2.6 Dhima za Nyimbo

Mulokozi (1996), ameeleza kuwa, nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa sana katika jamii za kiafrika. Hutumika kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko, kuonya, kufunza, kuarifu, kunogesha hadithi, kuomboleza, kubembeleza mtoto ilialale, kuchapuza kazi, na hata kutia hamasa vitani. Akizielezea nyimbo za nyiso, akiashiria nyimbo zote zinazoimbwa unyagoni au jandoni, ameeonesha dhima za nyimbo hizo ikiwa ni pamoja na kuwatia moyo wari, kujivunia kutoka hatua ya utotoni kuingia katika hatua ya utu uzima, kuyakabili maumivu ya kimwili na kuaga utoto. Utafiti huu unahusu kuchunguza dhima za nyimbo za ngoma ya msondo wa Pemba. Katika kazi ya Mulokozi, mtafiti amefaidika kwa kupata maarifa na urahisi wa kuchunguza dhima za nyimbo za msondo.

Msokile (1981) amesema kuwa nyimbo lazima zilingane na hadhira yake, ujumbe, mafunzo yanayotolewa kwa jamii ni lazima yafungamane na falsafa ya jamii husika kulingana na wakati na mahitaji ya jamii. Nyimbo hutumika katika kuelimisha wanandoa kuwa na maadili mema, unyenyekevu, utulivu, ustahamilivu, na hekima pamoja na adabu nzuri, ili kumjengea kuwa na sifa za kupendeza na kupendwa katika jamii.

Baadhi ya kazi tangulizi ambazo mtafiti ametalii ni, Sengo (1985), amechunguza mafunzo katika nyimbo za msanja wa Makunduchi. Matokeo ya utafiti wake ameonyesha kuwa, nyimbo za msanja wa Makunduchi hutoa mafunzo juu ya malezi

na maadili mazuri yanayomsaidia mwanajamii kujua namna ya kuishi kulingana na jamii yake.

Raya (2002) alichunguza nyimbo za harusi za wanawake waswahili wa Mombasa. Katika utafiti wake alijikita zaidi na mitindo kutokana na fonolojia, msamiati, semantiki na lugha iliyotumika. Utafiti wa Raya ulishughulikia zaidi katika kipengele cha lugha katika nyimbo hizo. Mtafiti alifaidika kwa kupata urahisi wa kuchambua vipengele vya fani katika nyimbo za ngoma ya msondo wa Pemba.

Haji (2005) na Saada (2007), wao walichunguza mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za harusi katika jamii ya Wazanzibari. Katika utafiti wao wameona kwamba nyimbo za harusi hutoa mafunzo kwa wanandoa katika kujenga, kuimarisha na kudumisha uhusiano, mapenzi na udugu katika ndoa zao. Pia wameeleza kuwa nyimbo zina nafasi kubwa katika kutoa mafunzo kwa bibi na bwana harusi namna ya kuishi kwa muda wao wote katika maisha ya ndoa. Mtafiti kwa kutalii kazi za watafiti hawa amefaidika kwa kupata urahisi wa kuchambua mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo wa Pemba.

Mdungi (2010), alichunguza nafasi ya mafumbo katika nyimbo za harusi. Katika kazi yake ameonyesha kuwa nyimbo za harusi zinatumia lugha ya ishara, taswira, tamathali za semi kama vile sitiari, tashbiha, tashhisi, tauria nakadhalika. Katika kazi hii mtafiti alifaidika kwa kupata maarifa ya kuchambua mafunzo ya nyimbo za ngoma ya msondo, na pia kupata urahisi katika kujadili vipengele vya fani katika nyimbo za msondo wa Pemba. Seif (2011), alichunguza dhima za nyimbo za jando na unyago katika jamii ya Kikaguru. Katika utafiti wake amebaini kuwa vijana

wanaopata mafunzo ya jando na unyago wao huonekana kuwa na maadili mazuri na wale wote ambaao hawakupata mafunzo wanakosa kabisa maadili mazuri katika jamii.

Katika utafiti wake alitoa ushauri wa jamii ya Kikaguru kurudia mila na dasturi za kuwapatia vijana mafunzo ya jando na unyago. Mtafiti amefaidika na kazi hii kwa kupata mwanga wa kutumia nadharia na namna ya kuchambua data zaa utafiti. Rashid (2013) alichunguza mafunzo ya nyimbo za jando na unyago katika jamii ya Wahiyao wa Masasi.

Katika utafiti wake aligundua kuwa nyimbo hizo lengo lake ni kuwaanda vijana waliofikia utu uzima kuishi maisha ya kiutu uzima. Aidha, aligundua kuwa vijana wanaopelekwa jandoni na unyagoni ni wadogo hawawezi kutunza siri za mafunzo na baadaye wanapokuwa huyafanyia majaribio mafunzo hayo na kupelekea kukosa maadili.Mtafiti wa kazi hii amefaidika na kazi hii kwa kupata urahisi wa kuchambua mafunzo ya nyimbo za msondo.

Silau (2013), yeye alichunguza dhima za nyimbo za Kikaguru katika kukuza na kuimarisha malezi kwa jamii ya Kikaguru. Matokeo ya utafiti wake ni kuwa nyimbo za Kikaguru zina nafasi kubwa katika kuimarisha malezi ya vijana wa Kikaguru, lakini alilogundua ni kuwa vijana wengi wa Kikaguru hawapendi nyimbo za ngoma za Kikaguru badala yake wanapenda miziki ya nje, kwasababu ya kuona aibu kucheza kwao. Aidha, vijana hao wametawaliwa na video, picha za mambo ya Ulaya, vijana wengi wanasimulia miziki ya magharibi tu tofauti na vijana wa zamani. Katika utafiti huu mtafiti kafaidika kwa kupata kutalii kazi tangulizi ambazo zilitumiwa na Silau.

Dominic (2013), amechunguza nafasi ya nyimbo za Kipare katika maisha. Utafiti huu ulifanyika tarafa ya Gonja Same. Matokeo ya utafiti wake aligundua kuwa, wanajamii wanaotumia nyimbo hizi zinawaelimisha na kuwaburudisha. Aidha nyimbo hizo zinwajengea wanajamii tabia njema, kuhifadhi amali za jamii yao, ziliwaonesha ukweli katika maisha, zilihifadhi lugha yao na ziliweza kuendeleza harakati za jamii dhidi ya mazingira na kujenga utaifa.

Na kwa wale ambao hawakuthamini nyimbo hizi walionekana kukosa maadili mema ya jadi. Kwa hivyo imebainika kuwa tatizo sugu la kushuka kwa malezi mema kwa jamii ya Wapare ni kutothamini nyimbo zao za jadi na kuendeleza kuzithamini nyimbo za kisasa. Mtafiti wa kazi hii amefaidika sana na kazi hii kwa kupata wepesi wa kuchambua dhima za nyimbo za ngoma ya msondo wa Wapemba.

Ndumbaro (H.T), amechunguza dhima na dhamira katika nyimbo za kabila la Wamatumbi. Katika utafiti wake ameonesha kwamba nyimbo za kabila la Wamatumbi, zina dhamira ya maadili mema, maonyo, umoja, mshikamano, kuelimisha jamii, kutoa mafunzo kama vile kuthamini kazi, kukataza ulevi, wizi na kuhimiza upendo. Katika kazi hii mtafiti amefaidika kwa kupata urahisi wa kuchambua dhima na mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo.

Kwa kutalii kazi tangulizi hizo, mtafiti alipata kianzio kizuri katika utafiti huu wa kuchunguza dhima za nyimbo za ngoma ya msondo wa Pemba. Mtafiti amenufaika na utalii huo wa kazi tangulizi kwa kujiongezea maarifa ya kuchambua kwa undani dhima na mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo. Na kwamba mtafiti amebaini kwamba hakuna utafiti uliofanywa juu ya uchunguzi wa dhima za

nyimbo za ngoma ya msondo wa Pemba. Kwa hivyo, mtafiti amepata wepesi wa kufanya utafiti huu ili kuziba pengo la tatizo la utafiti huu

## 2.7 Mkabala wa Kinadharia

Sengo (2009), Wafula (2007), Chimerah (1999), ñNadharia ni wazo kuu, fikira kuu, mwongozo mkuu, wa mtu au watu (jamii) wa pahala fulani wakati fulani, kwa sababu fulani. Nadharia ni miongozo inayomwelekeza mtafitiwa kazi ya fasihi. Nadharia inatufanya tufikiri, tusaili, tuweke tashwishi, na tuone ukweli. Nadharia inatoa mwanga na kuweka wazi kilichofichika.

Kwa jumla, tunaweza kusema, nadharia ni kanuni, taratibu, shariya, mwongozo, mwanga wa kukuelekeza juu ya namna jambo au kitu fulani kilivyo na kinavyokuwa. Kwa hivyo basi, nadharia ya utafiti ni mwongozo wa kufuata wakati wa kuchambua data za utafiti, huonesha maelekezo ya kufuata katika vitendo vya utafiti.

Nadharia zilizojadiliwa ni nadharia ya Uamilifu, nadharia ya Simiotiki, na nadharia ya Sosholojia. Mtafiti ametumia nadharia hizi katika kazi yake, kwasababu ndizo zinazokubaliana na kazi. Nadharia ya Uamilifu ilimwongoza mtafiti katika kuchambua dhima katika nyimbo za ngoma ya msondo. Nadharia ya Simiotiki, ilmwongoza mtafiti kufumbua fumbo na fumbuzi zilizotumika katika nyimbo hizo, na katika kuchambua vipengele vyengine vya fani. Dhima katika kazi ya fasihi haziwezi kuchambuliwa bila kuvitumia vipengele vya fani, vipengele vya fani ndivyo vinavyoibua maudhui katika kazi ya fasihi ikiwa ni pamoja na dhima na mafunzo.

### 2.7.1 Nadharia ya Uamilifu

Kwa mujibu wa Wamitila (2006), waasisi wa nadharia hii ni Franz Boaz, Bronislaw Malinowski na Radeliffe Brown. Nadharia hii inatazama zaidi dhima na dhamira ya kazi mbali mbali za jamii husika. Nadharia hii inasisitiza kuwa kazi yoyote ya fasihi ni lazima iwe na lengo fulani au ilenge kuleta ujumbe fulani katika jamii. Hivyo, waasisi wa nadharia hii, walitazama kila kazi ya fasihi au kipengele cha fasihi kina dhima gani katika jamii husika.

### 2.7.2 Nadharia ya Simiotiki

Mwasisi wa nadharia hii ni Frednard de Saussure. Anaeleza kwamba Simiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara au uashiriaji. Nadharia hii inatufundisha juu ya namna ya kufahamu, juu ya matumizi ya lugha ya ishara, kwamba yanarejelea nini katika kazi ya fasihi, lugha ya ishara inajenga misimbo gani katika kazi ya fasihi.

Nadharia ya Simiotiki ina misimbo ya aina tano, msimbo wa kimatokeo, msimbo wa kiheminitiki, msimbo wa kiurejelezi, msimbo wa kiseme na msimbo wa kiutamaduniò (Wamitila 2002). Msimbo wa kimatokeo: Kwa kutumia msimbo huu mtunzi anajenga visa, matukio, kwa njia ya ishara. Kwa mfano katika shairi la ôMbuga ya Kondooô Mvungi katumia mbuga ya kondoo kama ni ishara ya utumwa.

Msimbo wa kiheminitiki: Ni msimbo unaojengwa katika anwani ya kifasihi, anwani hiyo inaweza kuwa jina la kitabu, shairi, igizo. Kutokana na anwani hiyo tunaweza kufahamu mtunzi anarejelea nini katika kazi yake ya fasihi. Mfano Ebrahimu Hussein katika kazi zake, Mashetani, Ngao ya Jadi, Jogoo Kijijini katumia msimbo

wa kiheminitiki. Msimbo wa kiurejelezi: Msimbo huu hutumia maneno yenye kurejelea mambo mbalimbali ambayo yanauhusiano fulani na maneno wenyewe. Msimbo wa kiseme: Ni msimbo ambao unajenga maneno yenye kutowa maneno yenye maana ya kisemantiki. Msimbo wa kiutamaduni: Msimbo huu hujitokeza mtunzi anapotumia vitu vya asili vya utamaduni vyenye kurejelea dhamira mbalimbali. Mfano msanii anatumia nyumba za msonge, ukili, ukindu, ubuyu, vyungu, njuga na vyenginevyo.

### 2.7.3 Nadharia ya Sosholojia

Mwasisi wa nadharia hii ni Adam Smith, alianzisha nadharia hii 1970, huko Marekani. Bwana Smith anasema nadharia hii inajikita zaidi katika kuangalia uhusiano wa mwanaadamu na jamii yake. Msokile (1992), akifafanua nadharia hii anaeleza kuwa, nadharia hii huikabili kazi ya fasihi kwa kuangalia jinsi inavyohusiana na mazingira ya kijamii.

Nadharia hii huamini kuwa, uhusiano kati ya kazi ya fasihi na jamii ambayo kazi hiyo imeandikiwa ni muhimu sana. Anaendelea kufafanua kwamba, sanaa haijengwi katika Ombwe, ni kazi ya mwandishi katika mazingira na wakati maalumu akiwajibika kwa jamii inayomuhusu ambayo ni sehemu yake muhimu, mazingira ya jamii ndiyo huwezesha kubadili maudhui ya kazi ya fasihi.

Mtafiti ameteuwa nadharia ya Uamilifu, nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Sosholojia ambazo zilimwongoza katika kazi yake hiyo. Sababu za kuteua nadharia hizo ni kwasababu, zinazokubaliana na mada ya utafiti huo, ambao ni uchunguzi wa dhima katika nyimbo za ngoma ya msondo.

## 2.8 Sababu za Kuteua Nadharia

Mtafiti ameteua nadharia hizo kwa sababu ndizo zinazokubaliana na mada ya utafiti huu, nadharia ya Uamilifu hii inasisitiza kuwa kazi ya fasihi nilazima iwe na lengo na ujumbe fulani, kwa hiyo imetumika katika kuchambua dhima za nyimbo msondo. Nadharia ya Simiotiki hii imetumika kwa kuchambua vipengele vya fani, na nadharia ya Sosholojia imetumika kuangalia mafunzo ya nyimbo na hali halisi katika jamii. Na sababu kubwa zaidi ni kuwa kuzijuwa, kuzichambua na kuzitumiya nadharia nyingi ni muhimu kwa mzamili na mzamivu, kwani akifaulu kuipata M.A au PhD, atahitajika na yeye kuzifundisha nadharia kwa wanafunzi wake.

## 2.9 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti amejadili maana ya utalii, maana ya kazi tangulizi, maana ya nyimbo, aina ya nyimbo, dhima za nyimbo, mafunzo ya nyimbo, maana ya nadharia. Aidha nadharia tatu zimejadiliwa, nadharia hizo ni nadharia ya uamilifu, nadharia ya simiotiki na nadharia ya sosholojia, sababu za kuteuwa nadharia hizo pia zimeones

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi wa sura

Katika sura hii mtafiti kaonesha mbinu alizotumia katika kukusanya data za utafiti huu. Mbinu aliyotumia ni mbinu ya usaili, mbinu ya kushiriki na mbinu ya maktabani. Mtafiti pia kaeleza kundi lengwa, usampulishaji aliotumia kuwapata watafitiwa wa utafiti huu. Eneo la utafiti, maadili ya utafiti na mipaka ya utafiti, vifaa vilivyotumika katika utafiti pia mtafiti kaelezea katika sura.

## 3.2 Mbinu za Kukusanya Data

ñMbinu ya kukusanya data ni mbinu zinazotumiwa na mtafiti katika kupata data za utafiti wakeò (Daniel 2006). Anaendelea kueleza kuwa ziko mbinu tafauti ambazo zinaweza kutumiwa katika kukusanya data, mbinu hizo ni pamoja na uchunguzi makini, usaili, hojaji, majaribio, mahojiano ya vikundi nakadhalika. ñMbinu za utafiti ni mipango inayowekwa katika kukusanya na kuchambua taarifa kwa kupata ukweli, ili kusuluhisha jambo, kujibu swali la utafiti au kutatua tatizoò (Opie 2004).

ñNjia ya utafiti ni utaratibu mzima anaoutumia mtafiti katika kukusanya data za utafitiò (Kothari 1990). ñNjia za kukusanya data ni njia ya maktabani na njia ya uwandaniò (Opie 2004). ñNjia maktabani hutumia mbinu ya usomaji wa vitabu, majarida, magazeti, ripoti za utafiti katika vyuo vikuu nakadhalika, na njia ya kukusanya data kutoka uwandani hutumia mbinu za uchunguzi makini, usaili, hojaji, mahojiano ya vikundi nakadhalikaò. (Panneerselvan 2004). ñMbinu za utafiti ni utaratibu maalum unaopangwa kufuatwa ili kumuongoza mtafiti katika kukusanya na

kuchambua data za utafitiò. (Kothari1990). ñUkusanyaji wa data ni zoezi la awali la kupata taarifaò(Kothari 1990). Anaifafanua dhanna ya ukusanyaji wa data kuwa, ni zoezi la awali la utafiti, ambalo humwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye madhumuni yake ya utafiti. Aidha, mtaalamu huyo anasisitiza kwamba, hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data, hauwezi kufanyika kabla ya hii ya ukusanyaji. Hivyo basi, mtafiti alitumia mbinu ya usaili, mbinu ya kushiriki, na mbinu ya maktabani ili kupata data katika utafiti wake.

### 3.2.1 Mbinu ya Usaili

ñUsaili ni mbinu ya kukusanya data kwa njia ya mazungumzo ya ana kwa ana, baina ya mtafiti na mtafitiwaò (Babbie1999) na Omari (2001). ñUsaili kama mbinu ya kukusanya data, ni uulizaji wa maswali kwa mdomo na kujibiwa kwa mdomo piaò (Kothari 1990). Anaendelea kueleza kuwa, usaili huweza kuwa wa uso kwa macho baina ya muulizaji na muulizwaji, au huweza kuwa wa simu na hatimaye majibu hurikodiwa kirimbo au flash au katika daftari.

ñUsaili ni majibizano ya ana kwa ana, au ya simu, au ya barua pepe kati ya watu wawili au zaidi kuhusu suali fulani la kiutafiti lililoainishwaò, (Mulokozi 2006). Kwa mujibu wa Kothari (1990), faida za usaili ni pamoja na taarifa nyingi za undani hupatikana, taarifa zinazopatikana ni za uhakika kabisa. Usaili pia humwezesha mtafiti kuchagua watu wa kuwauliza maswali. Mtafiti anaweza kutaka ufafanuzi wa majibu pale ambapo, majibu ya watu anaowahoji hayaeleweki.

Mtafiti ameteuwa mbinu hii kutokana na faida za mbinu hii, na pia kutokana na maumbile ya mada ya utafiti huu na pia alihitaji kukutana na watafitiwa ana kwa ana

katika mazingira ya halisi. Mtafiti katika kutekeleza mbinu hii alitayarisha maswali ambayo aliwauliza watafitiwa wake nao walijibu kwa njia ya mdomo na mtafiti aliweka kumbukumbu zake katika kitabu chake alichokitayarisha kwa kukusanyia data za utafiti huu. Pia kwa kutumia mbinu hii watafitwa walipata fusa ya kuimba nyimbo ambazo wanazikumbuka.

### 3.2.2 Mbinu ya Kushiriki

Ushiriki ni ile hali ya kuungana pamoja kwa ajili ya kufanya jambo au kusaidiana katika shughuli au jambo fulani. TUKI (2004) na Enon (1998), wameeleza kuwa ushiriki ni mbinu ya ukusanyaji wa data kwa mtafiti kushiriki mwenyewe katika hali zote za kijamii. Hii ni mbinu inayovutia kwa mtafiti kwani kuna uwezekano wa kupata taarifa za moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa.

Mtafiti alishiriki katika shughuli ya harusi ambayo ilitayarishwa kwa ajili yake. Mtafiti alishiriki katika shughuli katika kijiji cha Chaleni katika shehia ya Mwambe, katika shughuli hiyo kulipigwa ngoma ya msondo na nyimbo nyingi ziliimbwa, mtafiti alipata fursa ya kuziandika nyimbo hizo zilizoimbwa katika shughuli hio.

### 3.2.3 Mbinu ya Maktabani

Mbinu hii inahusisha utalii wa kazi zilizofanywa na watafiti wengine waliotangulia.

Kazi hizo zinaweza kuhusu nadharia au dhanna zinazohusiana na mada ya utafiti (Kothari 1990). Mbinu hii ilitekelezwa kwa kusoma makala na vitabu kuhusu dhima za nyimbo ngoma tafauti. Maktaba zilizotumika ni maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania makao makuu Kinondoni, maktaba ya Chake chake Pemba na maktaba ya Chuo kikuu cha Taifa Zanzibar.

### 3.2.4 Kundi Lengwa

Kwa mujibu wa Kothari (1990) na Enon (1998), kundi lengwa ni mtu mmoja, kikundi cha watu, ambao mtafiti amekusudia kuwahusisha katika utafiti wake. Katika utafiti huu, kundi lengwa lilikuwa ni watu wazima wenye umri kati ya miaka 40-60 wanawake na wanaume wa kisiwani Pemba. Mtafiti aliteuwa watu wazima wenye umri huu, kwa sababu wazee hawa ndio wanaoelewa hasa nyimbo za ngoma hii ya msondo, kwa sababu ndio wanaoifahamu na kuiendeleza ngoma hii ya msondo.

### 3.2.2 Uteuzi wa Watafitiwa

Kwa mujibu wa Kothari (1990), uteuzi wa watafitiwa ni kitendo cha kuwapata washiriki wa utafiti kutoka katika kundi lengwa. Babie (1999), anasema, uteuzi ni sehemu ya idadi ya watu ambayo mtafiti anavutiwa nayo katika kupata taaifa za kutoa hitimishi la utafiti wake. Muller (1970), ameeleza sababu ya kutumia kundi dogo kuwakilisha kundi kubwa ni kupunguza gharama na kukidhi mahitaji ya muda.

Mtafiti alitumia uteuzi kusudio, uteuzi kusudio ni aina ya uteuzi ambao mtafiti huutumia katika kuchagua watafitiwa kwa madhumuni maalum, (Enon1998). Mtafiti alitumia uteuzi huo kupitia uteuzi tajwa, uteuzi tajwa ni uteuzi ambao mtafiti anapata taarifa kwa watu ambao hutajwa na wenzao, yaani mtu uliyemuhoji anamtaja mwengine ambaye anaweza kukupatia taarifa unazozihitaji. Mtafiti alitumia uteuzi huu kusudio alihitaji zaidi watu wazima kwa sababu ndio wanaozijua nyimbo hizo kwa undani kabisa na kwa upande wa vijana sio rahisi kutoa taarifa za nyimbo za msondo. Watafitiwa ishirini na saba waliteuliwa katika zoezi la kukusanya data za

utafiti huu, wanawake kumi na nane na wanaume tisa. Vijiji vilivyohusika ni tisa, kila kijiji walipatikana watafitiwa watatu wanawake wawili na mwanamme mmoja. Uteuzi huu ulifuata mawazo ya Kothari yanayodai kuwa, uteuzi nzuri uwe ni wa kati na kati, usiwe mkubwa sana walandogo sana.

### 3.4 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika shehia tatu, shehia za Kengeja, Mwambe na Mkungu, Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba. Katika shehia ya Kengeja, vijiji vilivyohusika ni kijiji cha Mkumbi, Kidishi na Mjiweni. Vijiji vya shehia ya Mkungu ni Mahuduthi, Mkungu na Sipwese. Katika shehia ya Mwambe, vijiji vilivyohusika ni Bwegeza, Mchakwe na Chaleni.

### 3.5 Maadili ya Utafiti

Katika utafiti huu, maadili ya kiutafiti yalizingatiwa ili kuhakikisha kuwa hakuna madhara yatakayotokea kwa washiriki. Maadili hayo ni pamoja na kwamba mtafiti alihakikisha kuwa ushiriki katika utafiti huu ulikuwa wa hiari na washiriki walikuwa huru kujiondoa katika utafiti huu wakati wowote bila kutakiwa kutoa sababu ya kujitoa kwao.

Kadri ilivyowezekana, utafiti huu haukuingilia ratiba za kazi za kila siku za washiriki wa utafiti huu. Mtafiti alijitahidi kuheshimu mila na dasturi za jamii katika maeneo ambayo utafi huu ulifanyika, na kwamba mtafiti hakufanya kitu chochote ambacho kilivuruga thamani ya mila na dasturi zao, juu ya yote haya muhimu ilikuwa ni makubaliyano kati mtafiti na watafitiwa wake na mambo yalikwenda vizuri.

## 3.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza dhima za nyimbo za ngoma ya msondo na sio nyimbo nyengine zozote. Lengo kuu la utafiti ni kuzikusanya nyimbo hizo na baadaye kuanisha mafunzo yanayopatikana kwenye nyimbo hizo kwa jamii, hasa kwa wanandoa na kwa watarajiwa wa ndoa. Na kwa upande wa vipengele vya fani vilivyoibua dhima na mafunzo kwa jamii, kipengele kilichojadiliwa ni kipengele cha matumizi ya lugha tu.

## 3.7 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti hutegemea aina ya utafiti, lakini aghlabu baadhi ya vifaa hivi ni kama kalamu na karatasi, shajara ya uwandani, tepurekoda na vifaa vyake, video/ kamera, rikodi na vifaa vyake, kamera na vifaa vyake, kompyuta na vikorokoro vyake, hojaji na dodoso, vifaa vya kupimia na kuhesabu, darubini, viona mbali nakadhalika.(Mulokozi 1983). Kothari (2004), ameeleza kuwa vifaa vya utafiti ni vyombo ambavyo mtafiti huvitumia katika ukusanyaji wa data. Kwahivyo, mtafiti katika utafiti huu ametumia vifaa kama vile, kalamu na karatasi, kompyuta, simu ya mkononi, flash, ngamizi. Vifaa vilivyotumika na jinsi vilivyoweza kumsaidia kama ifuatavyo:

### 1 Kalamu na karatasi

Kalamu na karatasi ni zana za msingi katika utafiti wa kitaalamu. Kalamu ilitumika kama nyenzo ya kuandikia majibu ya maswali ya utafiti ambayo mtafiti aliyauliza katika ukusanyaji wa data za utafiti. Karatasi nayo ilitumika kwa kuhifadhia data za utafiti zilizokusanywa katika maeneo husika ya utafiti.

**2 Kompyuta**

Kifaa hichi kilitumika kwa kutafutia data za utafiti katika tovuti. Aidha, data zilizokusanywa kutoka uwandani zilihifadhiwa kwenye kifaa hiki na baadaye kufanyiwa uchambuzi, ambao ulipelekea kupatikana matokeo ya utafiti huu. Mtafiti pia alitumia kifaa hiki kwa kuchapia kazi yake yote.

**3 Simu ya mkononi**

Mtafiti alitumia kifaa hichi kwa kupata mawasiliano kati yake na wataftiwa wake, hali hii ilimrahisishia mtafiti kupata data za utafiti.

**4 Flashi**

Flashi imetumika kuhifadhia data za utafiti na ripoti nzima ya utafiti huu, na kutumika wakati wowote zinapohitajika.

**5 Ngamizi**

Kifaa hiki kilitumika kwa ajili ya kuchapia kazi ya utafiti wa nyimbo. Aidha, ngamizi ilitumika kwa kuhifadhia data, kutafuta machapisho na maandishi kwa ajili ya kufanya utalii kupitia wavupepe.

## 3.8 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti kaonyesha mbinu zilizotumika katika kukusanya data za utafiti huu ambazo ni mbinu ya mahojiano, mbinu ya kushiriki na mbinu ya maktabani. Uteuzi wa watafitiwa uliotumika ni uteuzi kusudio ambapo uteuzi tajwa ndio uliongoza kupatikana watafitiwa wa utafiti huu. Eneo la utafiti, maadili ya utafiti, mipaka ya utafiti na vifaa vya utafiti vimezungumziwa katika sura hii.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusika na uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka uwandani na maktabani. Katika uchambuzi huu nadharia zilizotumika ni nadharia ya Simiotiki, Uamilifu, na nadharia ya Sosholojia. Uchambuzi huu utajibu maswali ya utafiti, je, ni zipi nyimbo za ngoma ya msondo? Je, ni dhima gani zinazopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo? Je, ni mafunzo gani yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo? Na Je, ni vipengele gani vya fani vilivyosaidia kuibua mafunzo hayo kwa walengwa?

## 4.2 Uwasilishaji wa Data

Baada ya mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa, watafiti wote wamekubali kuwa nyimbo za ngoma ya msondo zinatoa mafunzo mazuri kwa wanandoa na kwa jamii kwa jumla. Nyimbo zilizokusanywa ni ishirini na moja, hii ni kwasababu, watafitiwa wengine waliimba nyimbo zaidi ya moja na wengine walirudia nyimbo hizo hizo.

Dhima zilizojitokeza katika nyimbo hizo ni pamoja na dhima ya kuelimisha kwa kuonya, kukataza, kuhimiza, kuadilisha, kuburudisha, kuadabisha nakadhalika, ufafanuzi zaidi unaonekana kwenye uchambuzi wa nyimbo hizo. Mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo ni pamoja na ustahamilivu wa matatizo na shida katika maisha ya ndoa, utunzaji wa siri za ndoa, kumuenzi na kumdhibiti mume, kuwaheshimu wazee na jamaa wa mume, kuwacha tabia mbaya, kutunza usafi na kujenga tabia ya kujipamba na kujipodoa mke anapokuwa na mume

wake, mashirikiano na masikizano katika maisha ya ndoa, nakadhalika kama inavyoonekana katika uchambuzi wa nyimbo hizo. Nyimbo zilizokusanywa zinaonekana katika kiambatanishi namba mbili, hapa zimetajwa baadhi tu:

Wimbo 1: **Ulivyotaka kuolewa**

*Ulivyotaka kuolewa wee, utampara samaki wee*

*Samaki ana magamba wee, utampara samaki wee*

*Samaki ana vumba wee, utampara samaki wee*

*Samaki ana miba wee, utampara samaki wee*

*Samaki ana mashavu wee, utampara samaki wee*

*Samaki ana mapezi wee, utampara samaki wee*

*Bwa Mjuma wee, bwa Mjuma wee ana mliowe akuruza*

*Kurukurukuru ana mliowe akuruza*

Wimbo 2: **Raruwa dereva raruwa**

*Raruwa dereva, raruwa wee*

*Ulivyotaka kwa hiyari yako, utaupanda mlima*

*Mlima una mawe uwo, utaupanda mlima*

*Mlima una topeuwo, utaupanda mlima*

*Mlima wateleza uwo, utaupanda mlima*.

Wimbo 3: **Ushangia mapengo msumeno wangu**

*Ushangia mapengo, msumeno wangu wee*

*Kama haukerezi ntakwenda zangu wee*

*Mama ntaka karanga wee kaukarange na ule mdude*

*Kama hauna mafuta wee, kaukarange kwa maji ya kundee*

*Nikaukarange wapi wee, kaukarange chini ya gae*

Wimbo 4: **Ukitaka mume akae**

*Ukitaka mume akae wee, kutandika kuna maanae wee*

*Ukitaka mumeadumu wee, kutandika kuna maalumu wee*

*Ukitaka muume aishi wee, kutandika kuna maandishi wee*

*Ukitaka muume apende wee, umrambe kama peremende*

Wimbo 5: **Ila**

*Una ila moja ila, yako wewe bibi*

*Kusema nimechoka ila*

*Una ila moja ila, yako wewe ila*

*Ukisemezwa husemi ila*

*Una ila moja ila, yako wewe ila*

*Hutandiki kitanda ila*

*Una ila moja ila, yako wewe ila*

*Ukiondoka huagi ila*

Wimbo 6: **Bibi harusi tandika**

*Mama harusi tandika, tandika mgeni akae*

*Dada harusi tandika, tandika mgeni akae*

*Shangazi harusi tandika, tandika mgeni akae*

*Mgeni yoyoooo, tandika mgeni akae*

*Mgeni tunu ooo, tandika mgeni akae*

*Mgeni shoga ooo, tandika mgeni akae*

***Wimbo 7: Watu wote waolewa***

*Mama oooooo, ooooooo*

*Watu wote waolewa mie siolewi kwani*

*Una ila moja, wakojoa kitandani*

*Na ila ya pili, watukana majirani*

*Na ila ya tatu, wagombana na wahisani*

*Na ila ya nne, kutwa kiguu njiani*

*Kanijengee kibanda, kwetu Tundauwa*

*Washanigeuza mwendo, chepu wataniuwa*

Wimbo 8: **Mwari wangu wenda kwako**

*Mwari wangu wenda kwako, kuna mambongwa ukoo*

*Kuna mirimo mirimo, mabonde na mashimo*

*Usikute kijungu ufunuwe, kuna mambongwa ukoo*

*Usikute kitanda utanduwe, kuna mambongwa ukoo*

*Usikute mambongwa ukasema, kuna mambongwa ukoo*

*Kuna mirimo mirimo, mabonde na mashimo*

Wimbo 9: **Hongera mwanangu**

*Hongera mwanangu weee hongera*

*Nami nihongerae wee hongera*

*Mama uchungu mama uchungu*

*Nyamara mwanangu wee*

*Nyamara mwanangu chungu la udere*

*Linauma mno wee, lina uma mno hoya*

*Wimbo 10:* ***Mwana wapende wakwezo***

*Mwana wapende wakwezo, we ntoto hoya*

*Hizo kwako ndio nguzo, we ntoto hoya*

*Ujapopata tatizo, we ntoto hoya*

*Ni kimbilio la mwanzo, we ntoto hoya*

*Hoya ntoto hoya, hoya ntoto hoya*

## 4.3 Uchambuzi wa Data

**Utangulizi**

ñMboga yoyote inayochumwa kutoka shambani na kutupwa uwanjani bila kuchambuliwa si mbogaò. Hivyo basi data zimechambuliwa zikiongozwa ni nadharia ya Uamilifu, nadharia ya Sosholojia na nadharia ya Simiotiki.

Kutokana na mada ya utafiti na madhumuni ya utafiti huu, data zimekusanywa kutoka uwandani na maktabani, uchambuzi wa nyimbo za msondo ni kama ifuatavyo:

Dhima za nyimbo za msondo ni dhima ya kuelimisha na dhima ya kuburudisha kama hivi:

Kuelimisha kwa nyimbo hizo ni kuelimisha kwa kuonya, kuadilisha, kukataza, kuhimiza na kufundisha.

### 4.3.1 Dhima ya Kuelimisha

Dhima ya kuelimisha kuwapenda na kuwathamini wazazi na jamaa wa mke wako au mume wako ni, katika nyimbo ñ*kutaka kusudi kuolewa wee, utampara samaki*ò

Wimbo huu, wa utampara samaki, huimbiwa biharusi na bwana harusi, wakifahamishwa maisha ya ndoa sio maisha ya utotoni, maisha haya yana raha na shida zake, mwanamke anafahamishwa namna ya kuishi na mume wake pamoja na wazazi na jamaa wa mume wake, na mume naye, atambuwe mke ana wazazi na jamaa zake, kwa hivyo kila mmoja ajuwe kuwa wazazi wa mwenzake na yeye ni wake, kuwaheshimu, kuwapenda ni jukumu lao. Samaki ni mume au mke, magamba, mapezi, miba na vumba ni sehemu ya samaki, kwahivyo, ni ishara ya wazazi na jamaa wa mume au mke.

Kwa kutumia nadharia ya Uamilifu, wimbo huu una dhima ya kuelimisha kwa kufunza, kwahivyo wimbo huu umehusiana na nadharia ya Uamilifu, kwani nadharia hii inadai kwamba kazi ya fasihi ni lazima iwe na dhima au lengo katika jamii, na kwa kutumia nadharia ya Simotiki ñsamakiò ni ishara ya mume, kwamba mwanamke anafunzwa kuwa alivyomtaka mume huyo hana budi na kuwataka na jamaa wa mume. Magamba, vumba, miba, mapezi na mashavu ni sehemu ya samaki na wala haziwezi kutenganishwa naye na akaweza kuishi samaki huyo, kwa hivyo magamba, vumba, miba, mapezi ni ishara ya jamaa wa mume, mume amezaliwa na amelelewa, kwahivyo ana wazazi wake, walezi wake, jamaa zake, jirani zake, marafiki zake, kwahivyo mke ni jukumu lake kuthamini na kuwaenzi wazazi na jamaa wa mume wake, na kuwaona ni sehemu ya mume wake. Na mwanamme ni hivyo hivyo, wazazi wa mke wake ni wazazi wake, kuwaheshimu na kuwathamini ni jukumu lake.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia (Ujamii), dhima hii imo katika jamii zetu na ndio silaha ya ndoa zetu, kwa mke kuwajali na kuwathamini wazazi wa mume wake kwani, kwa kufanya hivyo ni kuzidisha mapenzi kati ya mume na mke, na mapenzi

katika ndoa ni silaha ya kulinda na kuhifadhi ndoa zetu. Kwa wanawake wanaopuuza mafunzo haya, ndoa zao huwa na misukosuko na huwa hazidumu, kwani kila mmoja anahitaji kupendwa na kupendewa wazazi wake na jamaa zake kwa jumla.

Dhima ya kuelimisha, kuwapenda wakwe, pia inapatikana katika wimbo usemao: ñ*Mwana wapende wakwezo"*. Wimbo wa ñmwana wapende wakwezoò, unafundisha maharusi, hasa biharusi, kuwapenda wakwe zake, kwani wao ndio watu wake wa karibu, katika maisha yake mapya. Wakwe zake ndio watu wa mwanzo ambao wataweza kukutatulia matatizo pindipo utapata matatizo.

Wimbo huu nao una dhima ya kumuelimisha bibi harusi anahimizwa kuwapenda wakwe zake, (mkwe kwa Kipemba ni mzazi wa mume au mke), kwa hivyo ni jukumu lake mke au mume kuwapenda wakwe zake, kwani wao ndiwo watakaomsaidia kwa raha na shida, kwamba wazazi wa mume wako au mke wako na wewe ni  wazazi wako. Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, dhima hii iko katika jamii za Wapemba na Wazanzibari kwa jumla. Na wala sio busara kwa mke kuolewa anapofika kwa mume, kuwadharau wazazi wa mume na jamaa zake kwa jumla na majirani pia. Wimbo huu unazidi kuelimisha, kwamba mwanamke anapofika katika familia ya mume, wazazi wa mume na jamaa zake ndio watu wake wa karibu, anatakiwa awe nao bega kwa bega, kwa hali yoyote ile, kwasababu wazazi wake wanakuwa mbali naye.

Dhima ya kuelimisha kwa kutunza siri na kuwawastahamilivu, inapatikana katika wimbo wa ñ*kakae mama kakae".* Wimbo huu, unamfundisha biharusi kwenda kukaa vizuri na mume wake, katika maisha ya ndoa hakuna mema matupu na shida zipo,

mke au mume hawana budi kuwa wastahamilivu, na wawe ni wenye kutunza siri za ndani ya ndoa yao, maisha ni kupata na kukosa, sio kupata tu.

Kwa kuongozwa ni nadharia ya Uamilifu, wimbo huu una dhima ya kuelimisha kwa kuwafahamisha mke na mume, kwamba maisha ya ndoa ni maisha yanayohitaji ustahamilivu mkubwa, kwani kuna kupata na kukosa, na juu ya hayo kunahitaji kutunza siri za nyumba yao, wasiwe ni wenye kutoa siri za nyumba yao. Wimbo huu unawaelimisha, kwamba katika maisha ya binaadamu, sio siku zote mtu anapata raha, kuna baadhi ya siku, mtu hupata matatizo. Hivyo mke anatakiwa aishi na mume wake kwa furaha na kutunza siri za nyumba yake. Iwe kupata au kukosa, mke aendelee kukaa na mume wake kwa furaha na heshima, amshukuru Mumba wala asikufuru. Anayetoa riziki na kunyima ni Allah. Hivyo, mke ni vizuri kukaa na kuwa na subira ya kusubiri riziki nyingine. Hivyo, wimbo, unaelimisha kuwa mke akipata au akikosa ni juu yake kutunza siri za nyumba yake na wala asiitangaze kwa watu wengine. Wimbo umesadifu nadharia ya Uamilifu, kwani inasisitiza kazi yoyote ya fasihi lazima iwe na lengo au ujumbe kwa jamii.

Wimbo wa ñ*Saada kaolewa*ò pia una dhima ya kuelimisha juu ya mafahamiano katika maisha ya ndoa. Mtafiti akiongozwa ni nadharia ya Uamilifu, ameuanisha wimbo huu, kuwa una dhima ya kuelimisha kwa kuwafundisha wanandoa na jamii kwa jumla kwamba, kitendo cha kuolewa si jambo la kutegemea kupata utajiri na kupata vitu vya thamani, bali ndoa ni masikizano na maelewano. Katika wimbo huu, neno ñuaò ni ishara ya mwanamke, kwa kutumia nadharia ya Simiotiki ñuaò ni mwanamke, kwamba mwanamke akitaka kuolewa kunataratibu zinapaswa

zichukuliwe, kwa mfano, hatua ya posa na hatua ya kutolewa mahari. Katika mshororo usemao:

*"Huko pwani kuna ua, la chanua kimanjano*

*Ukitaka kulichuma, ulichumie sindano"*

Mchoro huu, unafahamisha kwamba, mwanamke akitaka kuolewa lazima apatiwe mahari, lakini mahari hayo yasiwe makubwa kiasi ambacho mwanamme ashindwe, bali linalotakiwa hoja ni mafahamiano. Kama wimbo unavyoeleza:

*"Kuolewa si besera wee Saada wee*

*Hoja ni msikizano wee Saada wee''*

*"Besera''* ni aina ya kitanda maarufu hapo zamani ambacho kilikuwa na thamani kubwa kwa wakati huo (Bi Tijara). Bi Tijara akimwelezea mtafiti kuwa vitanda vya besera vilikuwa vikitumiwa zaidi na matajiri. Hivyo, wimbo unatufahamisha kuwa kuolewa si besera, bali ni masikizano. Kwa kutumia nadhari ya simiotiki, ñbeseraôô ni ishara ya utajiri, kwahivyo, wimbo unatufahamisha kwamba, kuolewa sio kupata utajiri au mali bali ni masikizano na mafahamiano mazuri kati ya mume na mke katika maisha yao ya ndoa.

Kwa kuongozwa ni nadharia ya Sosholojia, katika jamii ya Wapemba sio jambo zuri kwa wazazi wa mwanamke kudai mahari mengi kwa ajili ya mtoto wao, kwani jambo hili linapeleke kupata mateso mwanamke, kwani mwanamume huhisi kama amemnunua mwanamke huyo. Kwa hivyo, wimbo unatufahamisha kwamba masikizano ni jambo la muhimu katika maisha ya ndoa na sio mali wala utajiri.

Kuelimisha kwa nyimbo za msondo, pia kunajitokeza katika wimbo wa ñNdege huyoò

*Ndege huyo, mzuri kwa maua*

*Hata akipata uchanja, ndege atatua*

Wimbo huu unaelimisha kwa kumfahamisha msichana na wanawake wengine katika jamii, kwamba, mwanamke anawajibu wa kumtunza mume wake na mume naye anapaswa amtunze mke wake katika maisha yao ya ndoa. Kwa kuongozwa ni nadharia ya Simiotiki, neno ñndegeò ni ishara ya mume, na neno ñmauaôô ni ishara ya wanawake, kwa hivyo, wimbo unaeleza kwamba, mume anahitaji matunzo kwa mke wake, na mke anahitaji matunzo kwa mume wake, wanawake ni jukumu lao kuwatunza waume zao, na mume anajukumu la kumtunza mke wake, mume anavyoonekana, basi sifa zinakuwa ni za mke wake, na mke akitunzwa na mume wake, sifa ni za mume.

Ikiwa mume atakuwa msafi, sifa kwa mke na kinyume chake ikiwa mume ni mchafu basi sifa hiyo mbaya ni ya mke wake. Mume ni mzuri anapoenziwa, kudhibitiwa na kutunzwa na mke wake, hivyo ni wajibu wa mke kumtekelezea mume wake yale yote yanayomridhisha na yanayokubalika katika jamii na katika Dini ya Mola Karim. Kufanya hivyo, ni fursa adhimu ambayo ameipata yeye na kukoseshwa wengine, lakini akishindwa kutekeleza wajibu wake wa kumenzi mume wake na kumtunza, basi mume anaweza kushawishika na wanawake wengine au anaweza kuowa mke mwengine, kama wimbo unavyoeleza:

ñ*Hata akipata uchanja ndege atatua''*

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, neno ñuchanjaôô ni ishara ya mwanamke mwengine au matunzo mazuri, kwahivyo, wimbo unatufahamisha kuwa, mume anakuwa mzuri anapopata matunzo mazuri kutoka kwa mke wake. Mwanamke anapojifanya hana muda wa kumshughulikia mume wake na kumpa matunzo mazuri yanayomridhisha, mwanamme huyo anakuwa si rahisi kutulia kwake, muda mwingi huupoteza nnje kwenye mabaraza, na huenda akatafuta mwanamke mwengine akitarajia kupata matunzo mazuri yatakayomtuliza nafsi yake.

Kwa jumla, wimbo unatuelimisha wanawake wenye waume, wawe na mbinu nzuri za kimapenzi ambazo zitawavutia waume na kupata utulivu katika ndoa zao na kuweza kuishi kwa upendo na kudumisha ndoa zetu. Kutokana na elimu inayopatikana katika wimbo huu ni wazi kuwa wimbo huu unakubaliana na nadharia ya Uamilifu inayodai kuwa kazi yoyote ya fasihi ni lazima iwe na lengo fulani au ilenge kuleta ujumbe fulani katika jamii. Kwa kutumia nadharia ya Ujamii, elimu inayopatikana katika wimbo wa ñndege huyoò huu imo katika jamii, na hali hii, ni muhimu kwa jamii za Wapemba na Waswahili kwa jumla.

Dini ya Kiislamu imefahamisha hivyo, Mtume Muhammad (s.a.w), amesema, ñLau ningaliamuru yeyote kumsujudia yeyote, ningaliamuru mwanamke, kumsujudia mumeweò (Tirmidhiy). Wimbo mwengine wenye dhima ya kuelimisha kwa kuwafundisha wanawake namna ya kuwaenzi na kuwabembeleza waume ni wimbo usemao, ñ*Ukitaka mume akae”*

*Kwa mwongozo wa* nadharia ya Uamilifu, wimbo huo nao unatoa elimu juu kuwaenzi na kuwabembeleza *waume*, wanawake wenye waume ni jukumu lao

kuwaenzi waume, kufanya hivyo ni kudumisha mapenzi ya ndoa, na pia kuidumisha ndoa yao. Wimbo unawaelimisha wanawake umuhimu wa kutandika kitanda, kitandani ni pahala muhimu ambapo panahitaji unadhifu wa hali ya juu wakati wowote, kitanda kina nafasi katika maisha ya ndoa.

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, ñkutandika kuna maandishiôô hii inamaanisha kwamba kitanda kinaishara zake kinapotandikwa, ni juu ya mwanamke kuzifahamu na kuzitumia katika ndoa yake, baadhi ya ishara hizo ni matumizi ya mashuka, mwanamke anaweza kutumia shuka yeupe kumfahamisha mume kuwa leo mambo mazuri mume wangu, ninakuhitaji, lakini kitanda kikitandikwa shuka jekundu, ni ishara ya kuwa mambo mabaya mume wangu hali, hairuhusu, nina dharura ya kisheria. Wimbo unazidi kufahamisha kuwa, mume na mke wanahitaji kubembelezana kwa hali tafauti ili wazidishe mapenzi, mshororo unaosema:

ñ*Ukitaka mume apende umrambe kama peremende*ò maneno, ñ*umrambe kama peremende"* ina maana ya kuwa, mume na mke, anatakiwa abembelezwe kwa namna tafauti tafauti ili azidishe mapenzi kwa mke wake au mume wake. Kuaminiana na kuhurumiana, huzidisha ukaribu wa kujaliana, kuthaminiana na kufanyiana yaliyo muhimu maishani.

Kwa jumla, wimbo huu unaelimisha kuwa, kila kitu kina utaalamu wake, mwanamke anatakiwa awe na ujuzi wa kutunza na kutandika kitanda chake na kukipamba kwa mapambo na kubadilisha mashuka aina kwa aina, na kuepuka kabisa uchafu. Hali hii humsaidia mume kukaa na kuishi vizuri na kuzidisha mapenzi, kwani kitandani ni pahala pa starehe na mapumziko hivyo ni lazima pawe safi na penye kuvutia. Kwa

dhima hii, wimbo huu unakubaliana na nadharia ya Uamilifu inayodai kuwa kazi ya fasihi lazima iwe na dhima yake kwa jamii yake.

Dhima ya kuelimisha ustahamilivu kutokana na shida na matatizo ya ndoa, pia inajitokeza kwenye wimbo wa *"raruwa dereva raruwa wee*ò

Kwa kuongozwa ni nadharia ya Uamilifu, wimbo huo, una dhima ya kuelimisha wanandoa kuhusu maisha ya ndoa kwa jumla, kwamba, katika maisha ya ndoa hakuna mema matupu, kuna raha na pia shida zipo. Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, neno ómlimaô ni ishara ya maisha ya ndoa na maneno ñmaweò ñtopeò naòóuteleziò yote yanaashiria shida au matatizo katika maisha ya ndoa, kwa hivyo, wimbo unawafahamisha wanandoa kwamba, katika maisha ya ndoa, kuna shida na matatizo, kwa hivyo ni juu ya mke na mume kuwa wastahamilivu yanapotokea matatizo ya hapa na pale. ñMlimaò ni mnyanyuko wa ardhi ambapo mtu huupanda na kushuka. Mtu anayepanda, hupata hisia ya ugumu, uchovu wa mwili na pia, kuvuta pumzi kwa haraka. Mlima una kupanda na kushuka, hivyo unaashiria maisha ya ndoa yanaweza kuwa mazuri au mabaya, kwa hivyo, hapana budi mke na mume kujua hali hiyo na waweze kukabiliana nayo. Wimbo umeyabainisha matatizo hayo kiishara, ñmaweò ni vitu ambavyo huweza kumsababishia mtu madhara, mfano mtu anapotembea huweza akajikwaa kwa mawe na akaumia na anaweza akapata majeraha.

Hali hiyo humuelimisha mwanamme na mwanamke kuwa, kuna mambo yanayoweza kuwakabili, ambayo yanaumiza na kuithiri akili kimawazo, basi yanapotokea, waweze kustahamili, kwani ndio maisha. ñJiweò pia ni kitu kigumu sio rahisi kulivunja, mwanamme basi naye awe jasiri na aweze kuvumilia maovu yoyote

yanapotokea, na awe mgumu kama jiwe kutoa talaka, awe mstahamilivu na anapotoa uamuzi uwe wa uhakika. Kwa mwongozo wa nadharia ya Simiotiki, ñtopeò na ñuteleziò zinaweza kuwa na ishara nyengine, ñtopeò huweza kumchafua mtu kwani, ni mchanganyiko wa udongo na maji, mtu anapozikanyaga huweza kumrukia mpaka kichwani katika maisha ya ndoa ñtopeò huashiria aibu na fedheha zinazoweza kumpata mwanamme au mwanamke wanaposhindwa kuitunza ndoa yao ipaswavyo, ñuteleziò huweza kuwa, ishara ya kuvunjika kwa ndoa, wanandoa wanaposhindwa kuvumiliana basi ndoa huvunjika kwa urahisi. Mtafiti amezichambua dhima katika nyimbo hiikwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu inayosisitiza kuwa, kazi ya yoyote ya fasihini lazima iwe na lengo katika jamii yake.

Kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia, Wapemba ni wastahamilivu katika maisha ya ndoa, kwa hivyo, wanawake na wanaume wanatakiwa wawe wastahamilivu katika maisha yao ya ndoa, ikiwa katika hali ya raha au shida, uvumilivu ndio ngao. Katika jamii hali za maisha ya ndoa yanaonekana, wapo wanandoa wenye subira, lakini wako wasiokuwa na subira, talaka kwao ni nyepesi kama karatasi, hali hii sio nzuri na nyimbo zinatuelimisha kuwa wastahamilivu kwenye maisha ya ndoa.

Kama haitoshi, wimbo wa ñ*ushangia mapengo msumeno wangu"* nao una dhima ya kuelimisha wanandoa na jamii kuwa wastahamilivu kutokana na mashaka na matatizo yanayotokea katika maisha ya ndoa. Kwa kuongozwa ni nadharia ya Uamilifu, wimbo huo nao una dhima ya kuelimisha wanandoa kuwa wastahamilivu wanapopata matatizo. Kwa kutumia nadharia ya Fani na nadharia ya Simiotiki, ñmsumenoò ni ishara ya ñmumeò. Wimbo unafahamisha kuwa, msumeno una

mapengo na msumeno ukiwa na mapengo haupati yaani haukerezi mbao ya aina yoyote. Kwa kuwa msumeno ni ishara ya mume, hapana shaka ni mume asiye na nguvu, yaani hana nguvu za kiume, na ndio mwanamke akasema *"kama haukerezi nitakwenda zangu wee".*

Kwa hivyo, wimbo unaelimisha wanawake waliolewa na wanaotarajia kuoleawa kwamba tatizo hili lipo, inapotokezea hali hii, mwanamke asichukuwe hatua au uamuzi wa haraka, kinachotakiwa ni ustahamilivu, kwani hali hii huweza kusababishwa na vituko vya mashetani au woga wa siku ya harusi, au urogaji, pengine mume kafanyiwa uchawi, mwanamke anatakiwa awe mstahamilivu huku wakitafuta tiba ikiwemo tiba asiliya, kama wimbo unavyosema:

ñ*Mama nataka karanga wee, kaukarange na ule mdude*
*Kama hauna mafuta wee, kaukarange kwa maji ya kunde*
*Nikaukarange wapi wee, kaukarange chini ya gae"*

Wimbo una muelimisha mwanamke, kuwa mstahamilivu wakati anapokumbana na hali hiyo ya msumeno kuwa na mapengo, afanye juhudi na maarifa kadri ya uwezo wake, na wala asifanye papara ya kurudi kwao, kama wimbo unavyosema ñ*kama haukerezi nitakwenda zangu wee*ò, ustahamilivu ni bora mpaka hali ikiwa ni mbaya na tatizo halikutatuka basi hapo atafute ushauri kwa watu wazima. Mwanamke anatakiwa awe na hekima na ustahamilivu ili kutatua tatizo hilo bila ya kuondoka nyumbani kwa mume wake. Kwani endapo atatoa maamuzi ya haraka na kukimbia kwa mume itakuwa si jambo la busara. Kutokana na dhima hiyo, mtafiti anaona kuwa, wimbo unakubaliana na nadharia ya Uamilifu inayosisitiza kazi ya fasihi ni lazima iwe na lengo na ujumbe katika jamii yake.

Kwa mwongozo wa nadharia ya Ujamii, hali hii hutokezea katika jamii, na inapotokezea katika jamii za Wapemba, basi mwanamke akishathibitisha ndoa hiyo huvunjwa, kwani mwanamke atakosa haki yake msingi ya kimaumbile ambayo ni miongoni mwa faida za ndoa.

Dhima ya kuelimisha umuhimu wa kufunzwa maharusi na umuhimu wa mashirikiano wakati wa kuwafunza maharusi, imejitokeza katika wimbo, *Yuwapi wee, yuwapi mamaye harusi aje hapa tuhangaike naye".* Kwa kuongozwa ni nadharia ya Uamilifu, nyimbo hii ina dhima ya kuelimisha wanawake wanaoolewa kuhusu kumuheshimu mume, pia wimbo unaonyesha kwamba katika jamii watoto hawafundishwi na mtu mmoja, tumeona kwenye nyimbo ya óyuwapi wee yuwapi mamaye harusiô umewataja mama, bibi, shangazi, somo wa harusi wote wanakusanyika kwa kumfunza mtoto wao ili asiende kufedheheka.

Elimu inayopatikana katika wimbo huu ni kumuheshimu mume, kwamba mume ni mtu anayetakiwa kupewa heshima, na katika mambo yanayochangia mtu kuwa na heshima kwa mume wake ni pamoja na kumuita bwana, kama wimbo unavyosema katika mshororo huu: *"Ukiitwa ewe bibi uitikie bwana labeka". Mtafiti amechambua dhima za nyimbo hii akiongozwa ni nadharia ya Uamilifu, kwasababu nadharia hii inashughulikia na dhima katika kazi za fasihi.*

Pia wimbo unawaelimisha maharusi kuwa katika kumuheshimu mume pia ni kumridhia mume kwa kila analotaka, hii inafundisha wanawake kuwa mke anapoolewa ni wajibu wake kumtii mume wake kwa kila jambo linalokubalika kisheria ,kama vile kumtimizia haja yake ya matamanio, kumsikiliza maneno

anayokwambia na pia kuzifuata amri zake zinazostahiki kufuatwa. Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia(Ujamii), Wapemba jambo hili la heshima kwa mume ni jambo linalotiliwa mkazo, hii ni kwasababu Wapemba wengi wao wameathiriwa na utamaduni wa dini ya Kiislamu, Dini ya Kiislamu inawahimiza wanawake kuwa na ñtwaaò yaani utiifu na heshima kwa waume. Katika kulichunga hilo, ndipo mwanamke hufunzwa mafunzo ya namna tofauti ya kiwemo ya kumwita mume wake bwana, kama mshororo wa nyimbo unavyoeleza:

ñ*Ukiitwa ewe bibi, uitike bwana labeka"*

Na katika wimbo wa *"sanyombe, sanyombe mwanangu*ò dhima ya kuelimisha wanawake kuwaheshimu waume wao imesisitizwa, mwanamke anatakiwa amwite mume wake, kama mshororo wa nyimbo unavyoeleza:

ñ*Mume aitwa bwana, mwari wangu wee"*

Kwa kutumia nadharia ya Dhima na Kazi, wimbo unazidi kutoa elimu ya kuitunza heshima ya mume ikiwa ni pamoja na kumwita jina ambalo litampa heshima na furaha, kwa lengo la kudumisha ndoa zenye mapenzi ya dhati. Elimu nyengine ni kufundishwa kutandika kitanda na kumpokea mume anaporudi katika shughuli za kutafuta riziki, jambo la kumpokea mume ni jambo zuri na muhimu kwa jamii ya Wapemba. Hali hii imetokana na mila na desturi za asili za mdogo kumpokea mzigo mkubwa wake na kuupeleka panapohusika. Hivyo wimbo unatoa elimu kwa biharusi kuwa na heshima ya kumpokea mume wake. Kwa kutumia nadharia ya Ujamii, heshima hii ipo katika jamii, lakini kwa waliozugwa na usasa, heshima hii wanaipuuzia, ndio mapenzi katika ndoa zao yamepungua mke kumpokea mume

wake.Wimbo haukuishia hapo, pia unamuelimisha mwanamke, kumwaga mume wake kama wimbo unaposema:

*"Mume anaagwa mwari wangu wee"*

Mwanamke anatakiwa awe na heshima ya kumwaga mume wakati wowote anapotaka kwenda popote. Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, heshima hii ni lazima katika jamii nyingi za Wapemba.

Kwenye wimbo wa, *"mwari aingizwe chooni*ò, dhima ya kuelimisha maharusi kutunza usafi inapatikana, maharusi wanahimizwa usafi wa nyumba na mwili, kujitia manukato na uturi ilikuvutia na kumtia mshawasha mume ili apagawe, amwage mapenzi kwa kipenzi. Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, wimbo huu una dhima ya kuelimisha maharusi jambo la usafi na kujipamba, mwanamke anatakiwa awe msafi na mwenye kujipamba ili apendeze kwa mume wake na awe tayari wakati wowote akihitajiwa na mume wake, na wala sio vizuri kuijpamba anapotoka kwenda safari, kwani wanawake wengine hawajipambi wakiwa na waume zao lakini wanapotoka ndio wanajipamba.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, utamaduni wa kujipamba uko katika jamii za Wapemba na katika wimbo huu kumetajwa ñmarashiò, ñuvumbaò na ñudiò vitu hivi ni miongoni mwa vifaa vinavyotumika katika utamaduni wa Wazanzibari na Wapemba wakiwemo, vitu hivyo hutumika kama manukato kwa wanawake. Vitu hivyo hutoa harufu nzuri ya kunukia, kwahivyo huwa kivutio kizuri kwa mume. Kama tunavyojuwa kuwa udi na uvumba hutumika kwa kuchomwa katika moto na kutoa harufu nzuri ambayo hutumika kwa kufukiza nguo na chumba kizima na

kupelekea chumba kuwa na harufu nzuri na huwa kivutio kwa mume na kumfanya asicheze mbali. Udi hutiwa kwenye maji ya kukoga ili mwili unukie vizuri. Kwahivyo basi, maharusi wanapewa elimu ya kuvitumia vifaa hivi, ili kudumisha usafi wa mwili na wa nyumba kwa jumla. Tabia ya usafi kwa mwanamke humfanya mume kuwa karibu na mke wake na kumfanya asitamani wanawake wengine majiani, anapowaona wanawake wa nje wamejipamba hajali wala hashughuliki kwake anafanyiwa zaidi ya hivyo, lakini kinyume chake mke akiwa hana kawaida ya kujipamba, mume wake hutamani wanawake wa nje anapowaona wamejipamba na kupendeza.

Kwa hivyo, wimbo una waelimisha wanawake wenye waume, kuwa na tabia ya kuijpamba wakati wote wanapokuwa na waume wao ili kuwafurahisha na kuwapa utulivu wa nafsi zao, vyenginevyo waume watakaa kwenye vikao vya karata au maskani hadi saa sita za usiku. Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia (Ujamii), katika jamii wako wanawake wanaojipamba vizuri wakiwa na waume wao, lakini wako waliokuwa hawajipambi hawajuilikani wakiwa na kazi au wamepumua, wao wanaonekana wako kwenye pirika tu, kwahivyo wanawake wajenge tabia za kujipamba kwa waume wao ili kudumisha ndoa zao na kutuliza nafsi za waume wao.

Wimbo wa ñ*Jiwe, jiwe, jiwe limpambwa wee*ò nao una dhima ya kuelimisha juu ya umuhimu wa kujipamba na usafi kwa jumla. Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, ambayo inajikita na kuangalia dhima katika kazi ya fasihi, wimbo huu una dhima ya kuelimisha maharusi, umuhimu wa kujipamba na kujiremba wakiwa na waume zao. Kwa kutumia nadharia ya Fani, neno ñjiweò ni ishara ya mwanamke mwenye sura mbaya ambaye amekaa sana hajaolewa. Jiwe linavyoonekana ni kitu

kisicho sura wala umbo maalum, kwa hivyo, jiwe limefananishwa na mwanamke huyu, lakini mwanamke huyo baada ya kupambwa amependeza na anavutia.

Hivyo wimbo unatupa elimu ya kuwa mwanamke akijipamba anapendeza na kuvutia, kwahiyo wanawake wenye waume wajipambe vizuri wanapokuwa na waume wao kwani kujipamba kwao kutawapa utulivu wa nafsi waume wao na kuwawezesha wapumzike kutokana na kazi nzito za mchana wa kutwa, na pia kutulia nafsi zao kutokana na waliyoyaona njiani kutokana na wanawake mashangingi wanaojipamba kwa kutafuta wanaume ili wawachune. Hivyo wimbo unawaelimisha wanawake wenye waume wawe na tabia ya kujipamba na kujirebaremba mbele za waume wao, kwani mapambo huzidisha mapenzi, na mume huwa karibu na mke wake.

Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, wimbo huu pia una dhima ya kuwaelimisha wanawake wanaochelewa kuolewa wawe na subira kwani kila mja ana riziki zake, na mwenye kusubiri hajuti, kama wahenga wanavyotuambia, na mstahamilivu hula mbivu kama wimbo unavyotuambia:

ñ*Nekuwa nagamu, na mume wa mwanangu*

*Hejiokotea machakacha, leo kampata mchuchu wa haja"*

Wimbo unatueleza kuwa, wazazi wa mtoto walikuwa na hofu ya mtoto wao kupata mume, lakini leo wamefurahi mtoto wao kapata mume wa kujuilikana na mwenye manufaa *"hejiokotea machakacha"* mahakacha ni majani makavu ya mnazi ambayo husukwa kwa kuchukulia kitu kama vile nazi au muhogo, au majani makavu ya mgomba ambayo hutumika kwa kujengewa ua. Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki

neno ñmachakachaò ni ishara ya mwanamme asiye na mpango wowote, kutokana na hayo ina maana kwamba mtoto kapata mume wa manufaa na sio mume asiyekuwa na mbele wala nyuma (hahehohe), hii inaonesha faida ya kusubiri. Kwahivyo wimbo unatuelimisha kuwa, watoto wari wawe wastahamilivu na wenye subira iliwapate waume wenye manufaa na wenye tabia nzuri na wasivamie wanaumeó ñmasharo baroò kwa lugha ya vijana wa leo.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, elimu hii ni mashuhuri kwa Wapemba, na ndiyo asili yao kutoa mafunzo haya kwa wasichana wanaoolewa na wanawake wengine katika jamii. Mafunzo hayo hupatikana katika sherehe zinazofanywa kwa kufuata jadi, na matokeo yake hupelekea kudumu kwa ndoa. Mafunzo kama haya hayapatikani kwa zile shughuli zinazofanywa kwa kuiga mila za kigeni ambazo ziko kinyume na mila na desturi za Waswahili.

### 4.3.2 Dhima ya Kuonya

**Dhima ya kuonya tabia mbaya inapatikana katika nyimbo zifuatazo:**

*"Mama ooo, watu wote waolewa miye siolewi kwani".* Wimbo huu una dhima ya kuonya tabia mbaya kwa mwanamke anayeolewa, na kwa wanawake wengine katika jamii. Kwa kutumia nadharia ya Uamilifu, wimbo unatoa tahadhari ya kuacha tabia mbaya ambazo zinaweza kupelekea kuvunjika kwa ndoa jambo ambalo halipendelewi kutokea kwasababu zisizokuwa na msingi. Wimbo unaeleza kwamba mtu akiwa na tabia mbaya si aghlabu kuolewa, kwani anakiuka mila na desturi za jamii na jamii humhukulia yuko kinyume na jamii husika. Miongoni mwa tabia mbaya ambazo hazipendezi katika jamii kwa mke anayeolewa ni tabia ya ulimi na

kugombana na majirani pamoja na wahisani, haipendezi hata kidogo mwanaume kuwa na tabia hizi. Katika jamii za Wapemba, tabia hizi ni aibu na fedheha kubwa na mwanamke anayetokezea kuwa na tabia hizi hukosa mchumba wa kumuoa, na mwanamke aliyekwisha kuolewa basi ndoa yake huwa hatarini. Wimbo pia unatoa onyo kwa mwanamke aliyeolewa, sio vizuri wakati anapohitajiwa na mume wake kisheria kusema mie nimechoka, ni jambo baya, kwani humjui mume wako ana hali gani na amekumbana na jambo gani huko anakorejea.

Katika sheria ya ndoa mwanamke wa Kiislamu aliyeolewa anapata dhambi kubwa wakati anapoitwa na mume wake kwa ajili ya kustarehe naye na mwanamke huyo akakataa bila ya sababu za kisheria zinazokubalika kama vile kuwa hayuko tohara au anaumwa. Kwahivyo, kwa kutumia na nadharia ya Sosholojia, wimbo huu umesadifu katika jamii ya Wapemba, kwani wanawake wenye tabia hizi wako, kwa hivyo wenye tabia hizo ni vyema kujirekebisha ili ndoa zao zidumu na kuimarika zaidi na kuwa na mapenzi ya kweli katika ndoa zao.

Wimbo pia unaonya wanawake walioolewa kuwacha tabia mbaya ya kurandaranda ovyo mitaani kama unavyo eleza:

*"Na ila ya tano, kutwa kiguu njiani*ò, ni ila, tabia mbaya isiyopendeza katika jamii ya Wapemba, mwanamke aliyeolewa kurandaranda ovyo mitaani bila ya sababu ya msingi. Ni juu yake mwanamke aliyeolewa, kukaa ndani kwake na kutulia, na kutoa huduma kwa mume wake na watoto wake hii ni tabia nzuri na inayopendeza katika jamii ya Wapemba. Kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia, ambayo inasisitiza kuwa kazi ya fasihi ni lazima iwe inauhusiano na mazingira ya jamii, kwahivyo katika jamii za Wapemba wanawake waliolewa wanahimizwa kuwa na tabia nzuri,

na kuwacha tabia mbaya za kutukana majirani na wahisani, kurandaranda ovyo mitaani, na kubwa zaidi, ni mwiko na ila kubwa, mwanamke kuhitajiwa na mume wake, kukasema nimechoka, hali hii hupelekea kupunguza mapenzi katika ndoa na hata kupelekea ugomvi na kuvunjika kwa ndoa. Kwa jumla, wimbo unatuasa wanawake kutokuwa na tabia mbaya, na badala yake kuwa na tabia nzuri ambazo hupelekea kuwa na masikizano kati ya mke na mume wake, pamoja na jamii kwa jumla. Tabia nzuri huvutia wanaume na hupelekea mwanamke, kuolewa haraka na kinyume chake, tabia mbaya humkosesha mwanamke kuolewa. Wanawake tujipambe kwa tabia nzuri tuishi vizuri na waume wetu ili tupate radhi zao na radhi za Muumba wetu.

Dhima ya kuonya tabia mbaya, inajitokeza pia katika nyimbo, *"Mwari wangu wenda kwako".* Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu inayosisitiza kuwa kazi ya fasihi ni lazima iwe na ujumbe fulani kwa jamii, wimbo huu una dhima ya kuonya tabia mbaya za umbeya na kuchunguza mambo yasiyokuhusu, neno kijungu limetumika kama ni ishara ya siri za watu, basi mwanamke anayeolewa anaaswa kuwa huko anakokwenda kuna mambo ya watu yeye asiyashughulikie wala akiona vitu vya watu asivipapie, na anapopewa siri za watu asizitowe kwa watu hali hii itakuwa ni tabia mbaya na itampelekea kuwa mwanamke mbaya mtaani na katika jamii kwa ujumla.

Kwa kawaida mtu anapoolewa anapofika kwake hukaribishwa na hukabidhiwa kwa watu, ndugu na majirani ambao hutarajiwa kuunga udugu na mashirikiano baina yao, kwa kusaidiana kwa hali na mali. Hivyo basi mtu anapokwenda kwa watu anatakiwa ajilinde na kuchunguza mambo ya watu na anapohitaji kitu chochote basi aombe

ruhusa kwa wenyewe ili apate kitu hicho anachokihitaji. Wimbo unaeleza kwamba mtu asiseme mambo ya watu, asizungumze siri za watu na wala asipeleleze mambo na shughuli za watu. Tabia hizo zote ni mbaya na hazipendezi katika jamii na ni aibu kubwa kwa mke kuolewa kujipamba na tabia chafu hizo.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, ambayo inaangalia kazi ya fasihi ilivyohusiana na jamii, kwa wanawake wa Kipemba kwao ni ila mwanamke kwenda mji wa watu akawa mbeya, mpekepeke na mchunguzi wa mambo ya watu yasiyomuhusu, na akisikia siri za watu akazitangaza hadharani au kwa watu wengine.

Wimbo unaendela kwa kumuonya mwanamke pia, katika maisha ya ndoa akiwa kwake na mume wake kuna mambo mengine ni siri hayatakiwi kuzungumzwa nje, ni tabia isiyotakiwa kabisa kwa mwanamke kutoa siri za nyumbani kwake, katika mshororo*, "Kuna mirimo mirimo, mabonde na mashimo, kuna mambongwa ukoo"*

Kwa mwongozo wa nadharia ya Simiotiki, inayoshughulikia lugha ya ishara katika kazi ya fasihi, maneno, mirimo, mirimo, mabonde na mashimo ni ishara ya kuwa katika ndoa kuna mambo ni siri baina ya mke na mume wake, kwa hivyo ni aibu mke kusema siri za mume wake na mwanamme kutangaza aibu za mke wake, au kwa upande mwengine sio vizuri kwa wanandoa kusema mambo wanayofanyiana ndani kwao, ni vizuri kutunza siri za ndoa.

Kwa jumla, wimbo unawaasa wanawake walioolewa kuwacha tabia ya umbeya, upekepeke na uropokaji wa mambo ya watu na mambo yao ya ndani katika ndoa zao, wanawake wenye tabia kama hizo huwa hawapendezi katika jamii na katika ndoa

zao huwa na dosari kubwa na hupelekea kukosa waume kutokana na tabia mbaya. Dhima ya kuonya tabia ya kuwadharau waume imejitokeza katika nyimbo za msondo, mfano kwenye wimbo, *"Bei ya nazi mwijua"*

Kwa kutumia nadharia ya Uamilifu, wimbo huu, una dhima ya kuonya wanawake kuacha tabia ya kuwadharau waume. Wimbo unawonya wanawake kuwacha kabisa kuwadharau waume, kwani hali ya maisha ni ngumu, wanaume wanahagaika kutafuta maisha ambayo ni magumu, kutokana na ongezeko la bei za bidhaa nyingi ambazo zinahitajika kila siku.

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki ñkigozi manyoyaò ni ishara ya starehe ya ndoa, yaani mwanamke anaaswa tabia ya kumnyima mume wake starehe ya ndoa bila ya sababu ya msingi inayokubalika kisheria, kwani lengo la ndoa ni kupata utulivu wa nafsi kwa mke na mume. Wanawake wengine wanakuwa hawaelewi majukumu yao katika ndoa kwahiyo huwa na tabia chafu za kuwanyima waume wao haki zao, kwahivyo wimbo huu una wakataza wanawake wenye tabia hizo kuziwacha kwani, zinawaathiri wanaume na hupelekea wanaume hao kuingia katika makosa ya kutafuta vimada, wakati wake zao a ndoa wapo, lakini wameshindwa kutimiza majukumu yao.

Wimbo unaeleza kuwa hali ya maisha ni ngumu, waume wanahangaika kutafuta mahitaji ya lazima kwa familia zao kutwa wanazungumka huku na kule, hivyo wanawake wenye kuolewa ni juu yao kuona hizi hali na kuwajengea mazingira mazuri waume wao wanaporudi majumbani, ili waume hao watulie majumbani, wakiwa na furaha na mapenzi kwa wake zao, hali hii itapunguza talaka za haraka na

kupunguza idadi ya wajane na wanawake wanaodhurura ovyo mitaani. Kutokana na dhima hiyo ya wimbo huo, hapana shaka wimbo unakubaliana na nadharia ya Uamilifu inayosisitiza kuwa kazi ya fasihi ni lazima iwe na dhima kwa jamii yake, mtafiti amechambua dhima hiyo kwa kuongozwa ni nadharia hii. Dhima ya kuonya wanawake kuwacha tabia mbaya hadi kufikia kutajwa vibaya, imejitokeza katika wimbo wa ñ*Nilikwenda pwani wee, mwiba wa ngogo ukanicho"*

Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu inayosisitiza kuwa kazi ya fasihi ni lazima iwe na dhima katika jamii, mtafiti ameuchambua wimbo huu kuwa una dhima ya kuonya maharusi na wanawake wengine katika jamii kuwacha tabia mbaya, kwani humpelekea mtu kutokubalika katika jamii na kuonekana ni mtu asiye na mila wala dasturi za Wapemba ambao wengi wao wanaonekana na tabia nzuri. Mwanamke anatahadharishwa na tabia mbaya ambazo zitapelekea kutajwa yeye mtaani kwa tabia zake mbaya kama wimbo unavyoeleza:

*"Mwanaadamu havumi, uvumao ni mwamba na ngoma"*

*Wimbo unawaasa* wanawake wanapofika mitaani, waache kabisa tabia mbaya za kuchukiza na kutajwa vibaya, bali ajipambe kwa tabia nzuri na sifa nzuri ili awe mfano wa kuigwa kiamboni. Kwahivyo, wanawake walioolewa na wale wanaotarajiwa kuolewa wanaaswa kuwa na tabia mbaya zitakazowafanya kukosa waume na kuwa wazururaji mitaani.

Kwa kuongozwa na nadharia ya Sosholojia (Ujamii) ambayo inaiangalia kazi ya fasihi ilivyosawiri jamii yake, Wapemba sio watu wenye tabu, kwahiyo wimbo unaonyesha ukwao wa Wapemba na wanahimizana kuzienzi sifa zao hizo kutoka

kizazi hadi kizazi chengine, kufuata mila na dasturi za watu kutapelekea kutia madoa sifa nzuri za wanawake wa Kipemba, halahala kizazi cha leo kuzienzi sifa za wanawake wa Kipemba.

Wimbo wa ñ*Hodi, hodi, hodi ya mwana mirambo”* ina dhima ya kuonya wanawake kuwacha tabia mbaya ya usesa na ufisadi. Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, wimbo huu una dhima kuonya maharusi na wanawake wengine katika jamii, kwamba mgeni anapofika mtaani anatakiwa taratibu za wenyeji wake, ikiwa ni pamoja na kukaa na kuishi na watu vizuri kama alivyowakuta watu wanakaa na kuishi, na asiwe yeye mgeni aliyefika ndiye chanzo cha ugomvi na kuwafanya watu wagombane na wahasimiane. Hivyo basi, wimbo unakataza tabia mbaya za kugombanisha watu na kuanzisha uhasama na kutenganisha watu, kama wimbo unavyosema *“mgeni havunji kiambo”* bali yeye awe ni chanzo na mwenye kuendeleza mahusiano mazuri aliyoyakuta ikiwa ni pamoja na kuishi vizuri na majirani pamoja na jamaa na marafiki wa mume wake.

Tabia hizi katika jamii za Wapemba zinapigwa vita, mtu mwenye tabia za upekepeke na ugomvi huwa hana nafasi katika jamii, watu humchukia na kumtenga kama hakujirekebisha na tabia zake mbaya, kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia, wimbo huu umeakisi mila na desturi za Wapemba. Kwa mwongozo wa nadharia ya Simiotiki inayoangalia ishara katika kazi ya fasihi zinarejelea nini, ñhodi, hodi, hodiôô, hodi hizi ni ishara ya mgeni kuingia katika viambo vya watu, katika jamii za Wapemba mgeni akiingia pahali huhitaji kukaribishwa, na wenyeji huwa ndio wenye jukumu la kumkaribisha mgeni huyo. Kwahivyo, mgeni huyo akishazoea asiwe ni mwenye kugombanisha watu katika mtaa huo.

Nyimbo ya *Videge viwili* inaonya wanawake kutokana na wanaume wa nje, wimbo huo una eleza kwamba wanandoa wanatakiwa wawe na mapenzi ya dhati, kwani lengo kuu la ndoa ni kuwa na maisha ya uhakika na yenye mapenzi ya dhati.

Wimbo unafafanua kuwa kuna videge viwili vitakufata kwa matamanio, kwa mwongozo wa nadharia ya Simiotiki, *"videge viwili"* ni ishara ya wanaume wa nje, ambao kwa kawaida hujinadhifisha na kuvalia vizuri ili wawavutie wanawake wanaowataka kimapenzi. Wimbo huu unaendelea kwa kumtahadharisha mwanamke, kuwa asiwe kiruka njia, abaki na mume wake wa ndoa, yeye ndiye aliyemchagua na kumuoa kutoka kwao na awache kabisa kutamani wanaume wa nnje. Mwanamke anatakiwa awe na mapenzi ya dhati kwa mume wake na asikubali kuhadaliwa na wanaume wa nje. Kutokana na dhima ya nyimbo hii, ni wazi kuwa wimbo umekubaliana na nadharia ya Uamilifu inayosisitiza kazi ya fasihi kuwa na dhima katika jamii yake.

Wimbo wa ñmaromaò nao unasisitiza swali zima la uaminifu na mapenzi ya dhati katika ndoa. Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, wimbo huu una dhima ya kumuonya mwanamke aliyeolewa, kuwacha kupumbazwa na wanaume wa nje, kwani wanaume hawa wanahadaa, wala hawana ukweli, mapenzi yao humalizika mara tu baada ya kupata wanachokitaka kwa mwanamke.

Kwa kutumi nadharia ya Simiotiki, neno ñ*maroma"* huashiria wanaume wa nje, ambao mwanamke anapaswa kuepukana nao, na badala yake abaki na óbabindo wakeô ikiwa ni ishara ya mume wake wa ndoa, kwani ndiye aliyebeba dhamana ya kumlisha na kumvika.

Kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia inayoangalia kazi ya fasihi na jamii, tatizo hili lipo katika jamii, kuna baadhi ya wanawake wanawaacha waume wao wa ndoa  na kushawishika na wanaume wa nje. Hivyo basi Wapemba pamoja na wanawake wa Kiswahili kuishi na mume wake ni jambo la furaha na kinyume chake, mwanamke kuwa na kimada pembeni sio mila wala desturi za waungwana.

Wimbo unaeleza zaidi kwamba, mwanamke anatakiwa amtegemee mume wake katika huduma zote katika maisha yao ya ndoa, kama mavazi, makaazi na kula, ijapokuwa kusaidiana ni jambo zuri na linakubalika, lakini si kutafuta wanaume wa nje, wimbo unaeleza kwamba:

ñ*Kama si babindo wangu ndani, ningali lala na njaa"*

Msisitizo mwengine wa kuonya wanawake walio kwenye ndoa kutoshawishika na wanaume wa nje ni katika wimbo huu: *'Huko pwani kuna mti, waitwa mgome gome'* Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, wimbo huu una dhima ya kuonya wanawake kuepuka kabisa wanaume wa nje, kwani hali hii hupelekea wanawake kuwadharau waume wao na kuthamini waume wa wenziwao, jambo ambalo huweza kusababisha matatizo makubwa katika ndoa na hata kuvunjika kabisa kwa ndoa hizo.

Wimbo unaeleza kwamba mti unaotaka kuchangwa una masharti ambayo ni lazima mtu asome jinsi ya kuuchanga, hapana shaka mti ni ishara ya mume, mtu anapoolewa lazima afundishwe namna ya kuishi na mume wake, mambo gani afanye na mambo gani asifanye ili kulinda ndoa yao. Hivyo wimbo unakataza kabisa mwanamke kuchukua waume wa wenzake. Neno óukomeô lina maana ya kumtaka mtu ache tabia fulani ambayo anayo mara moja. Katika utamaduni wa Kipemba

linapotumika neno hilo huwa ni amri inayotakiwa kutekelezwa halan. Wimbo huu unamuonya mwanamke aache tabia ya kuchukua waume wa wenziwe, kwani katika jamii halikubaliki.

#### 4.3.3 Dhima ya Kuburudisha

Kama ilivyo fasihi ina dhima ya kuburudisha, nyimbo za msondo nazo hazikuacha kubeba jukumu hilo, licha ya kutoa elimu na kuonya mambo yasiofaa na bourudani hupatikana. Mfano wa nyimbo zenye dhima hiyo ni wimbo wa *hauririmi msondo.*

Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, wimbo huu una dhima ya kuburudisha, maneno hauririmi yana maana ya haunogi au hauchapuki, ikiwa na maana ya kuwa, ngoma hii haiwi nzuri kama hakuwepo bibi Saumu, bi Saumu huyu alikuwa ndiye mwimbaji na mtungaji wa nyimbo nyingi za ngoma hii ya msondo, kwa hivyo alipata umaarufu kutokana na ngoma hii mpaka kutungiwa nyimbo hii ikiwa ni sehemu ya burudani.

Wimbo mwengine ni *mmaliwa, mmaliwa*. Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, wimbo huu una dhima ya kuburudisha, inaonyesha furaha kwa wazazi na jamaa wa mtoto kwa mwana wao kuolewa akiwa katika hali ya usalama. Maneno *mwenzenu kashaolewa leo aja chukuliwa* ni dalili ya furaha na burudani kwa wazazi na walezi. Wimbo wa *mliyosema hayawi mbona yamekuwa* pia una dhima ya kuburudisha, wimbo unasema: *Mliyosema hayawi, mbona yamekuwa.*

Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, wimbo huu umeingia katika kundi la nyimbo zenye dhima ya kuburudisha, ijapokuwa kuna mafumbo na vijembe

wanapigwa wambeya na mafisadi waliokuwa wakitia vidomodomo vyao katika ndoa hiyo, lakini mwisho ya yote ndoa imekuwa na watu wanashangilia, kwahivyo wimbo umebeba dhima nzito ya kuwatahayarisha mafisadi lakini pia una sehemu ya kutoa burudani.

## 4.4 Mafunzo Yanayopatikana Katika Nyimbo za Ngoma ya Msondo

Mtafiti akiongozwa ni nadharia ya Uamilifu inayosisitiza kuwa kazi yoyote ya fasihi ni lazima iwe na lengo au ujumbe kwa jamii, mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo ni kama yafuatayo:

### 4.4.1 Mafunzo ya Ustahamilivu wa Shida na Matatizo Yanayotokea Katika Maisha ya Ndoa

Nyimbo zenye kutoa mafunzo hayo ni *raruwa dereva raruwa wee.* Kwa mwongozo wa nadharia ya Simiotiki, neno dereva ni ishara ya mwanamme anayeowa au mwanamke anayeolewa, neno ñmlimaò ni ishara ya ndoa, yaani mwanamke amekubali kuolewa na mwanamme amekubali kuowa, kwahivyo, mwanamke na mwanamme hawana budi kuwa wastahamilivu kwa mambo yoyote yanayoweza kutokea katika ndoa yao, kwenye maisha ya ndoa hakuna mema matupu na matatizo yapo. Kama wimbo unavyoeleza*: Mlima una mawe huo utaupanda mlima, Mlima unatope huo, utaupanda mlima, Mlima wateleza huo, utaupanda mlima'*

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, maneno mawe, tope na utelezi yanaashiria shida na matatizo yanayotokea katika maisha ya ndoa, kwahivyo ni juu ya wanandoa kuelewa kwamba, katika maisha ya ndoa ukiachia raha na starehe zinazopatikana, shida na matitizo huweza kujitokeza bila kutarajia, kwahivyo wimbo unatoa mafunzo

kwa wanando kuwa wastahamilivu yanapotokea, mke awe mstahamilivu kwa mume wake na mume awe mstahamilivu kwa mke wake. Neno mawe ni ishara ya matatizo katika ndoa, hivyo mwanamke ni juu yake kuwa mstahamilivu, na kwa upande wa mwanamme afahamu kuwa, katika maisha ya ndoa kuna matatizo ambayo huenda yakasababishwa na mke wake, lakini kama lilivyo jiwe mume anatakiwa awe mstahamilivu na roho ngumu kama jiwe. Na kwa jumla wimbo unatoa mafunzo kwa maharusi kuwa wastahamilivu na wenye subira yanapotokea matatizo katika maisha yao ya ndoa, hali hii itaimarisha ndoa yao na itadumu katika hali ya mapenzi miongoni mwao na wala hasidi au adui hatopata nafasi, kama wanavyosema wahenga, ñwawili wakipendana adui hana nafasiöö.

Kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia inayoangalia kazi ya fasihi ilivyosawiri jamii yake, mafunzo yanayopatikana katika wimbo huu, yanaonekana katika jamii zetu, mara nyingi ndoa zinazofungwa kwa kufuata utamaduni wa kufundishwa maadili, kwa kutumia asili na jadi zetu aglabu zinadumu kwa muda mrefu, lakini ndoa zinafungwa kwa kuiga mila na tamaduni za kuiga, kama sherehe maholini, ñmahina party, ñkitchen partyò mara nyingi ndoa hizo hazidumu, kwasababu mafunzo yanayosaidia maharusi hayapatikani kwa kutumia mila na desturi za kuiga. Aidha neno ótopeô ni ishara ya shida na matatizo katika maisha ya ndoa, kama zinavyoonekana tope zinachopeza, mtu akizikanyaga anachopea na anaweza kuchafua nguo zake au anaweza kuanguka chini.

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki neno ñtopeò tunachukulia ni matatizo katika ndoa, matatizo huweza kuwa madogo au makubwa, ni juu yao wanandoa kustahamiliana na kuvumiliana. Pia neno ótopeô tunawaeza kusema ni ishara

matatizo katika ndoa yanayoambatana na aibu na fedheha kwa wanandoa hasa kwa mwanamke, kwahivyo anafundishwa bwana harusi kwamba, kwakuwa amemtaka mke huyo basi ni juu yake kustahamili kutokana na hali yoyote atakayoikuta juu ya mwanamke huyo, na mwanamke ni juu yake kuwa mstahamilivu juu ya hali yoyote atakayoikuta kwa mume wake, kwasababu amemtaka mwenyewe, kwahivyo akikuta raha au shida za maisha aone ni sehemu ya maisha. Neno óuteleziô nalo ni ishara ya matatizo, kama tunavyojua utelezi unapelekea mtu kuanguka chini, kwahivyo katika wimbo huu ni ishara ya kuvunjika kwa ndoa kunakosababishwa na matatizo na mashaka katika ndoa.

Hivyo basi wimbo unawafunza maharusi kujua kwamba, katika maisha ya ndoa kuna matatizo na shida, lakini kusubiri ni jambo la msingi, kwani wahenga walisema, ñsubira huvuta kheriò na ómwenye kusubiri hajutiô na kwenye maneno ya Allah, Allah anasema, ñInna Laha maa swabirinò, ikiwa na maana hakika ya Allah yupo pamoja na wenye kusubiriôö. Kwa mafunzo hayo, wanandoa tuweni wastahamilivu na wala tusiwe wepesi kuzivunja ndoa zetu kwa mambo madogo madogo tu, hususan wanaume wasiwe wepesi kuzitoa talaka kama hakuna sababu ya msingi inayokubalika kisheria.

Wimbo mwengine wenye mafunzo kama hayo ni: ñUshangia mapengo msumeno wangu weeò. Kwa mwongozo wa nadharia ya Simiotiki ambayo inaangalia ishara katika kazi ya fasihi inarejelea nini, msumeno ni ishara ya mume na mapengo ni ishara ya kukosa nguvu za kiume na nataka karanga yaani mwanamke anataka starehe za ndoa na pia pametumika taswira kama vile, maji ya kunde na chini ya gae, vipengele vyote hivyo vya fani, vinaibua mafunzo ya kustahamili kutokana na

matatizo yanayotokea katika ndoa, katika wimbo huu, mke anafunzwa kuwa, kuna wanaume wenye maumbile tofauti kwahivyo ni juu yake mwanamke kuyakabili, katika wimbo mafunzo yanayopatikana ni kuwa, mwanamke anapoolewa na akamkutia mume ana matatizo ya ukosefu wa nguvu za kiume, basi awe mstahamilivu kwani huenda tatizo hili limetokana na woga, au ni maswali ya kishetani.

Mwanamke awe mstahamilivu huku akitafuta dawa kwa wenye taalimu ya tiba. Nahaitaku jambo zuri kwa mwanamke kurudi kwao siku hizo hizo, kwani siri itafichuka na huenda ni tatizo la muda mfupi tu na linaweza kutibika. Mafunzo haya yapo katika jamii, kuna wanawake wanaoweza kustahamili lakini wengine hawezi kabisa kustahamili, kwa hivyo wimbo umesawiri jamii kama nadharia ya Sosholojia inavyosisitiza kuwa, kazi ya fasihi ni lazima iangalie mazingira ya jamii yake.

### 4.4.2 Mafunzo ya Kumuheshimu na Kumuenzi Mume au Mke

Mafunzo ya kumuheshimu na kumuenzi mume au mke yanapatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo, mifano ya nyimbo hizo ni: ñ*Yuwapi eee yu wapi mamae harusi aje hapa tuhangaike naye"*. Kwa mwngozo wa nadharia ya Uamilifu ambayo inasema kazi ya fasihi ni lazima iwe naujumbe kwa jamii, wimbo huu basi unatoa mafunzo ya kumheshimu na kumuenzi mume na pia juu ya umuhimu wa mashirikiano ya wazazi juu ya kumfunza mtoto wakati anapopata mume. Mafunzo ya kumuenzi na kumuheshimu mume yanaonekana katika mishororo inayosema:

*"Ukiitwa na mumeo mama wajibu kumuitika*

*Ukiitwa ewe bibi uitikie bwana labeka,*

*Umridhie mumeo, mama kwa kila analotaka".*

Mishororo hii ya wimbo huu, inatoa mafunzo kwa mwanamke namna ya kumuitikia mume wake, yaani anafundishwa aiitikie labeka bwana, hali hii inamtukuza mume na kujihisi kweli ni mume na pia ni kiongozi wa familia. Bi Tijara akinifafanulia mafunzo ya nyimbo hii alinieleza kuwa, wazee wa zamani na enzi zao, jambo hili hawakulifanyia ajizi, waume wao waliwaita bwana hata mbele za watu, lakini leo kwa kisiingizio cha maendeleo, wanawake wanaona tabu kuwaita waume wao bwana. Na badala yake huwaita baba yake fulani au kaka, vyereje mume kuwa kaka maajabu makubwa, kwahivyo wimbo unatoa mafunzo waume wawe waume na kaka awe kaka. Aidha wimbo unafundisha kuwa mwanamke anatakiwa kuwa na utii juu ya amri za mume wake ilimradi ziwe ni amri zinazokubalika kisheria na zisiwe zinazopindukia mipaka ya Allah (S.W).

Kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia, mafunzo haya yanayopatikana katika wimbo huu yamo katika jamii hususan kwa jamii za Wapemba ambao wengi wao wameathiriwa mno na imani ya dini ya Kiislamu, kwani Uislamu unahimiza wanawake wenye waume kuwatii waume wao ikiwa ni pamoja na kufuata amri na miongozo wanayopewa, kwani wanaume ni viongozi wa wanawake, kama Kurani inavyosema, ñArijaluu Kawamuna aala Nissai é é é é é é é é é é (Nnisai: 24), kwamba wanaume ni viongozi wa wanawake.

Aidha wimbo unatufunza kuwa katika kumpa mafunzo mtoto ni lazima wazazi washirikiane, kwani mtoto hafunzwi na mtu mmoja, kama wimbo unavyosema: *“Mama yake harusi twamtaka aje hapa, Shangazi yake harusi twamtaka aje hapa, bibi yake harusi twamtaka aje hapa, Na somo yake harusi twamtaka aje hapa, tuje tumfunze mwana asende kufedheheka’’*

Mishoro hiyo inaonesha wazazi wanavyoitana ili wampe mtoto mafunzo juu ya maisha ya ndoa ili asende kufanya viroja huko anakokwenda, mama, bibi, shangazi na somo wa harusi ni watu muhimu kwa kutoa mafunzo kwa mtoto, ili aelewe majukumu yake kwa mume wake, na kwa jamii kwa jumla. Hivyo basi mafunzo kwa maharusi ni jambo muhimu, na jamii isidharau mila na desturi hizi kwa kutumia taasisi husika kama jando na unyago, ngoma za asili ikiwemo ngoma ya msondo, wanawake na wanaumme waishi vizuri na waume wao, na kuwa na maadili mazuri, hali ambayo itapelekea ndoa zao kudumu na kuwa na mapenzi miongoni mwao. Nyimbo nyengine yenye mafunzo juu ya kumuheshimu na kumuenzi mume ni: *"Sanyombe, sanyombe mwanangu wee"*

Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu ambayo inasisitiza kuwa kazi ya fasihi ni lazima iwe ujumbe kwa jamii, wimbo huu ambao maneno yaliyotumika ni ya kawaida yaani maneno yake ni mepesi, unatoa mafunzo kwa maharusi wa kike kuwa, mume anaitwa bwana, jina ambalo linampa heshima na furaha ndani yake, mume akiitwa bwana anajisikia na hujenga mapenzi na mke wake, kwahivyo, wanawake walioolewa au wanaotarajia kuolewa wawaite waume wao bwana kama mshororo wa wimbo unavyotueleza: mume aitwa bwana mwari wangu wee.

Aidha mafunzo mengine yanayopatikana katika wimbo huu ni kuwa mume hutandikiwa kitanda, kama inavyoeleweka kitandani ni sehemu muhimu kwa maisha ya ndoa, pia ni miongoni mwa mambo yanayojenga heshima na mapenzi kwa mume. Kitanda kinapotandikwa kikatandikika, basi ni pumbazo kwa mume na huweza kumvutia mume na kumfanya abakie ndani muda mwingi na kuepuka kuzurura ovyo mitaani, kitanda pia humvutia mume na kumfanya kila wakati atamani kustarehe na

mke wake. Hivyo basi biharusi hufundishwa, kuwa mume hutandikiwa, kama mshororo wa wimbo unavyosema: ñmume atandikiwa mwari wangu weeò

Aidha, kumpokea mume anaporudi kazini au hata kondeni ni jambo linalojenga heshima kwa mume, mwanamke anatakiwa anapomuona mume wake kabeba mzigo, na mzigo huo anauweza basi ni jukumu lake mwanamke kumpokea mume wake. Kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia, suali hili la kumpokea mume ni jambo muhimu na linajitokeza katika jamii za Wapemba hasa kwa wale walifunzwa kupitia nyimbo za msndo, kwani jamii hii imejengeka na maadili ya kuwa mdogo humpokea mkubwa, hivyo wimbo umesawiri jamii.

Aidha mafunzo mengine muhimu yanayopatikana katika wimbo huu, ni kwa mwanamke kuomba ruhusa kwa mume wake anapotaka kwenda safari yoyote ile iwe safari kubwa au hata ndogo ni juu yake kuomba ruhusa kwa mume, funzo hili kwa kweli linaonekana kupewa nafasi kubwa katika jamii ya Wapemba. Kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia, mafunzo haya ni katika utamaduni wa Waswahili, Wapemba wakiwemo, na mwanamke ambaye anamwona mume wake anakuja na mzigo akafanya kama hamuoni, hili ni kosa na inakuwa ni dharau, kwahivyo wimbo umeakisi jamii yetu.

### 4.4.3 Mafunzo ya Kumuenzi na Kumdhibiti Mume au Mke

Mafunzo ya kumuenzi na kumdhibiti mke au mume yanapatikana katika nyimbo kama hizi: ñ*Ndege huyo, nzuri kwa maua", hata akipata uchanja, ndege atatua'*

Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu inayosisitiza kuwa kazi ya fasihi ni lazima iwe na lengo fulani kwa jamii, mafunzo yanayopatikana katika wimbo huu ni

kumtunza na kumdhibiti mume. Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki inayoangalia lugha ya ishara katika kazi ya fasihi inarejelea nini, vipengele vilivyoibua mafunzo hayo ni lugha ya ishara ambapo neno ñndegeò ni ishara ya mume na neno ómauaô ni ishara ya mwanamke na neno óuchanjaô ni ishara ya matunzo au mwanamke mwengine ambaye ana mapenzi ya dhati na matunzo ya uhakika.

Hivyo basi, wimbo unatoa mafunzo kwa maharusi na kwa wanawake walioolewa, kuwa waume wanahitaji matunzo na kushughulikiwa kwa kupewa mapenzi ya dhati na kuenziwa, waume sio watu wa kuwadharau, na endapo mwanamke atashindwa kumuenzi na kumdhibiti mume kwa kumpa mapenzi ya dhati, mume huyo atatafuta mke mwengine ambaye anahisi atampatia matunzo na mapenzi ya dhati, kama mshororo wa wimbo unavyosema: *"Hata akipata uchanja, ndege akatua".* Na kwa upande mwengine mke naye anastahili kuenziwa na kutunzwa na mume, na endapo mwanamme atashindwa kumtnza mke wake ndoa inaweza kutetereka, kwahiyo mke amtunze mume na mume amtunze mke wake.

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, uchanja ni ishara ya mwanamke mwengine mwenye mapenzi ya dhati na atakae muenzi na kumshughulikia kadri ya uwezo wake. Kwa jumla wimbo unatoa mafunzo kwa wanawake kwamba, mume anakuwa nzuri anapoenziwa, kutunzwa, kushughuikiwa na kudhibitiwa na mke wake, na kinyume chake, mke akishindwa kumtunza na kumuenzi na kumdhibiti mume wake, mume atachukuliwa na wanawake wengine au mume atatafuta mke mwengine ambaye anatarajia kupata huduma nzuri, ikiwa ni pamoja na matunzo na mapenzi ya dhati.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia inayoangalia kazi ya fasihi inavyohusiana na jamii, mafunzo haya ni mazuri, na wako wanawake katika jamii zetu wanayatumia, lakini wako wengine wanayadharau, hali ambayo ndoa za wanawake wanaowatunza waume wao zinakuwa imara na kuwa na mapenzi madhubuti, na kinyume chake kwa wanawake wanaoyapuuza mafunzo haya ndoa zao zinakuwa sio imara wala hazina mapenzi ya dhati na mara nyingi huwa hazidumu kwa muda mrefu. Wimbo mwengine unaotoa mafunzo ya kumuenzi na kumdhibiti mume ni: *"Ukitaka mume akae, kutandika kuna maanae"*

Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, wimbo huu unatoa mafunzo kwa maharusi juu ya umuhimu wa kutandika kitanda ikiwa ni sehemu ya kumuenzi na kumdhibiti na kumbembeleza mume na kumpumbaza kwa mapenzi. Kwahivyo, mwanamke ni juu yake kuwa makini katika nyumba yake, na kuwa makini na utunzaji wa kitanda. Raha na starehe ya ndoa huzidi mara dufu iwapo mazingira ya kitanda yako imara na yenye kuvutia.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, Wapemba kwa kuelewa umuhimu wa kitanda, hutoa mafunzo haya kwa maharusi wao ili kuwajengea mazingira mazuri katika ndoa zao. Wimbo unaendelea kutoa mafunzo juu ya umuhimu wa kitanda kama ni njia mojawapo ya kumuenzi na kumtunza na kumdhibiti mume, na kwamba kwa kutumia kitanda, mke anaweza kuwasiliana na mume wake, kama mshororo wa wimbo unavyosema: *"Ukitaka mume aishi, kutandika kuna maandishi''*. Mafunzo ya mshororo huu ni kwamba, mwanamke anaweza kutumia mashuka kama ishara ya kitendo fulani, kwa mfano kutandika shuka jeupe, kijani, manjano ni ishara ya kuwa, leo bwana mambo mazuri au ninakuhitaji, lakini shuka jekundu ni ishara ya kuwa,

leo bwana mambo sio mazuri, lakini kutokana na sababu za kisheria zinazokubaliwa. Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, neno maandishi ni ishara ya kuwa, kutandika kuna dalili zake au ujumbe wake, mwanamke na mwanamme ni vizuri kuzijua ishara hizo.

Wimbo unaendelea kwa kuzidi kutoa mafunzo juu ya kitanda kama ni njia ya kumuenzi na kumtunza mume na pia kumbembeleza mume, katika mshororo unaosema: ñ*Ukitaka mume apende, umrambe kama peremende"*. Hapa wimbo unawafundisha maharusi kwamba, katika kumuenzi mume ni kutumia njia za kumpumbaza kimapenzi kwa kutumia mbinu za kumfurahisha na kumtia hamasa ya mapenzi na kumvutia kwa kutumia mitindo ya kila aina ambayo inazidisha mshawasha kwa mume wake, ili kuzidisha mapenzi na maelewano kati yao.

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, maneno umrambe kama peremende ni ishara ya mitindo ya kumbembeleza mume kama vile kumsinga, kumchuwa kwa mafuta na kumkogesha, mambo hayo huzidisha mapenzi na kumvutia mume na pia kumdhibiti na kumfanya asitamani mwanamke mwengine wa nje ya ndoa yake.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, mafunzo haya ni mazuri na katika jamii za Wapemba, wako wanawake ambao huyatumia mafunzo haya na wamefanikiwa kuwatuliza waume wao, na wanawake wengine wanayadharau, ndoa zao hazina mwelekeo mzuri waume wao wanahangaika mara mwanamke huyu mara yule. Kwa jumla, wimbo unamfunza mwanamke awe na tabia za kumbembeleza na kumuenzi mume wake, kwani kufanya hivyo kunampelekea mume kujenga mapenzi zaidi na

mke wake, na pia kumfanya mume kubaki nyumbani na mke wake na kuwacha kuzurura ovyo mitaani bila sababu yoyote.

### 4.4.4 Mafunzo ya Utunzaji wa Siri za Maisha ya Ndoa

Mafunzo ya kutunza siri katika maisha ya ndoa yanapatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo. Nyimbo zenye mafunzo hayo ni kama: ñ*Kakae mama kakae, kakae na mume.*

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, wimbo huu umetumia lugha ya kawaida kwa kufikisha mafunzo kwa maharusi. Na kwa kutumia nadharia ya Uamilifu, wimbo huu unatoa mafunzo kwa biharusi ya kutunza siri za ndani katika maisha yao ya ndoa. Katika maisha ya ndoa kuna mambo mengi mazuri na mabaya, lakini wanandoa wanatakiwa wawe ni wenye kutunza siri, na wawe wastahamilivu juu ya yote. Katika maisha ya ndoa, kwa kuwa binaadamu sio mkamilifu wa kila kitu, basi kuna siku mtu anapata riziki za kumtosheleza, lakini kuna siku riziki zinakuwa hafifu, kwahivyo ni juu yake mwanamke kuwa mstahamilivu na mwenye kutunza siri hizo, kwani kupata na kukosa ni kazi ya Allah (S.W), na pia kheri na shari zote zinatokana na Allah Mtukufu.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, katika jamii za Wapemba mafunzo haya ni muhimu na yanasisitizwa sana, na wako wanawake wanaoyatumia mafunzo hayo, mtu anaweza kupata na shida na matatizo na akaweza kustahamili bila ya kumzungumzia mtu yoyote, lakini wanawake wengine ni aibu, siri za nyumba ziko hadharani hawawezi kutunza siri zao hata kidogo. Kwahivyo, ni vizuri mtu kukaa na kuwa na subira ya kusubiri riziki alizoandikiwa, na anapopata ashukuru na

anapokosa pia ashukuru wala asikufuru, anapopata anapokosa iwe ni siri yake ndani yeye na mume wake na wala asitowe nje kwa mashoga zake au majirani zake.

Wimbo mwengine unaofunza maharusi kutunza siri za maisha ya ndoa ni: *"Mwari wangu wenda kwako kuna mambongwa ukoo"*. Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, ambayo inasisitiza kuwa kazi ya fasihi ni lazima iwe na mafunzo kwa jamii, wimbo huu unatoa mafunzo kwa bibi harusi kuhusu kutunza siri katika maisha ya ndoa, siri hizo ikiwa ni ndani kwake na mume wake na hata za majirani zake. Katika maisha ya ndoa, kuna siri ndani yake, sio vizuri kwa mke wala mume kuzitoa siri hizo. Kwa mfano mambo ya ndani ya ndoa sio vizuri mke kuhadithia, kuwa mume wangu ananifanyia hivi na hivi, au mume pia kuhadithia marafiki zake mke wangu ananifanyia hivi na hivi, kama wanafanyiana mambo mazuri ni juu yao kupongezana wao wenyewe. Na kwa nje sio vizuri mwanamke kusikia mambo ya watu akawa yeye ndiye mtangazaji wa siri za watu, mtu anapoona mambo ya watu anaangalia macho tu, kwani kutangaza mambo ya watu ni tabia mbaya.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, tabia za kutoa siri za ndani na kutangaza mambo ya watu ambayo hayakuhusu ni tabia mbaya ambazo hazikubaliki katika jamii, ni tabia zinazokwenda kinyume na mila na dasturi za Wapemba. Katika jamii ya Wapemba, mwari aliyefunzwa akafunzika, basi ni mwiko kutoa siri za ndoa yake, na hata ukimwona mtu anatoa siri za ndoa yake basi hakufunzwa akafunzika kwa jina jengine huitwa msungo.

Kwa mwongozo wa nadharia ya Simiotiki, maneno *'kuna mirimo mirimo mabonde na mashimo*ôni ishara ya kuwa, katika maisha ndoa kuna siri nyingi, kwahivyo ni juu

yao maharusi kutambua hayo na kuweza kuzidhibiti siri hizo. Mambongwa ni mambongwa yaani ya mke na mume, na pia mke na wakwe zake, mambongwa kwa mke na majirani zake. Kwahivyo, kwa jumla, wimbo unawafunza maharusi na wanawake wenye waume, kujenga tabia ya kutunza siri za ndoa na pia kuwacha kushughulikia mambo ya watu na kutangaza siri za watu mtaani.

#### 4.4.4 Mafunzo ya Kutunza Usafi wa Mwili Pamoja na Kujipamba na Kujirembaremba kwa Wanawake wenye Waume

Wanawake wenye waume wanatakiwa kujenga tabia ya kujipamba na kujirembaremba kila wakati, ili kuwatuliza waume wao na kuwafanya wabaki majumbani kupata mapumziko baada ya kazi ngumu za mchana wa kutwa. Nyimbo zilizoibuwa mafunzo hayo ni pamoja na: ñ*Mwari aingizwe chooni, kwa maulidi”*

Kwa mwongozo wa nadharia ya Simiotiki, maneno uvumba, udi, marashi ni ishara ya usafi na kujipamba kwa mwanamke aliyeolewa. Lugha ya picha pia imetumika, maneno, mwari aingizwe chooni kwa maulidi, hii ni taswira inayojengeka na kuonesha kuwa, chooni ni pahala panapotumika katika kujitayarisha na usafi.

Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, inayosisitiza kuwa kazi ya fasihi ni lazima iwe na lengo kwa jamii yake, hivyo mtafiti akiongozwa ni nadharia hii ameuanisha wimbo huu kuwa, unatoa mafunzo kwa wanawake wenye waume, kutunza usafi na kujipamba na kujirembaremba wanapokuwa na waume wao kwani kufanya hivyo kunazidisha mapenzi katika ndoa, na mume anakuwa anajisikia fahari na anabaki nyumbani muda mwingi, na anaepukana na kuzurura ovyo mitaani. Pia katika kujenga tabia hiyo ya kujipamba na kujirembaremba, wanaume wanapata utulivu wa

nafsi zao, wanapokutana na wanawake wanaojipamba na kuzurura mitaani kwa lengo la kujiuza na kutapeli wanaume wasiotosheka, na ambao wake zao hawana kawaida ya kujipamba na kujirembaremba wanapokuwa na waume wao.

Mafunzo haya yanayopatikana katika wimbo huu ni mazuri na yamo katika jamii, inapaswa wanawake kuyatia akilini, kwani matatizo yanatokea katika jamii zetu, wanawake wanaojiachia tu bila kujipamba na kujirembaremba, waume wao wanahangaika kwa kutamani wanawake wengine ambao wanatabia ya kujipamba majiani, na hatari zaidi wanaume hao mara hufanya nao mapenzi, kwasababu wanavutika na mapambo yao. Kuna wanawake, hawajui kujitia hata wanja seuze hina au rangi za mdomo, na kwakweli wanawatesa waume wao.

Wanawake wengine hawajipambi mpaka wanapotoka kwenda harusi au mijini, tabia hii sio nzuri, wanawake wajipambe wanapokuwa na waume wao. Wanawake wengine wao hawajipambi mpaka wanapopata wakewenza yaani waume wao wanapotafuta wake wengine, hapo tena hujitiatia ushindani, basi wimbo unakufunza ewe mwanamke mwenye mume jipambe kwaajili ya mume wako umtulize nafsi yake, na wewe utuliye na mume wako, ili ndoa yako iwe na mapenzi na idumu daima dawamu. Kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia, mafunzo haya yamo katika jamii zetu, kwa hivyo wimbo umesawiri jamii.

Wimbo mwengine wenye mafunzo kama hayo ni: ó*Jiwe, jiwe, jiwe limpambwa wee”*. Kwa kutumia nadhari ya Simiotiki, jiwe ni ishara ya mwanamke ambaye amechelewa kuolewa, au mwanamke mwenye sura mbaya, ambaye akipambwa hupendeza vizuri. Kwa kupitia kipengele hiki cha fani, mafunzo yaliyooibuka ni

kuwa wanawake wenye waume wajenge tabia ya kujipamba na kujirembaremba wanapokuwa nyumbani na waume wao. Kwa kuongozwa ni nadharia ya Uamilifu, wimbo huu unatoa mafunzo kwa maharusi kujenga tabia ya kujipamba na kujirembaremba wanapokuwa na waume wao, isiwe wanapambwa siku ya harusi tu, iwe ni kawaida yao, ili wawatulize waume wao na wawaepushe na kutamani wanawake wa nje. Maneno herini na wanja ni viashiria vya mafunzo hayo ya kujipamba, kwani herini na wanja ni vifaa vinavyotumiwa na wanawake kujpambia.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, katika jamii ya Wapemba, wako wanawake wenye tabia hii ya kujipamba na kujirembaremba wakiwa na waume wao, tunawasihi waendeleze tabia yao hiyo. Lakini pia kuna wanawake wengine wao hawajui kabisa kujipamba, basi kwa mafunzo ya wimbo huu tunawasihi wajenge tabia ya kujipamba na kujirembaremba wakiwa na waume wao, kwani Waswahili husema ñijapokuwa kisiki cha mtema ukikipamba kinakaa vyemaò msemo huu una maana yakuwa, hata mwanamke akiwa mbaya vipi, basi akijipamba hukaa vizuri na kupendeza. Kwahivyo wanawake kwa mafunzo ya wimbo huu, tujipambeni ilituimarishe ndoa zetu na kuwatuliza nafsi zao waume wetu, ili tuwaepushe na vishawishi vya akina changu doa.

### 4.4.5 Mafunzo ya Kuwapenda na Kuwathamini Wakwe na Jamaa wa Mume au Mke

Nyimbo za ngoma ya msondo pia hazikuacha kutoa mafunzo kwa maharusi na wanawake wenye waume juu ya kuwapenda wakwe na jamaa za mume. Nyimbo zenye kutoa mafunzo hayo ni: *"Mwana wapende wakwezo, we mtoto hoya'.* Kwa kutumia nadharia ya Uamilifu, wimbo huu unatoa mafunzo kwa maharusi na

wanawake wenye waume, kuwapenda wakwe zao na jamaa za waume wao, kwani hawa ndio watu wake wa karibu anapokuwa na raha na pia anapopata matatizo. Wakwe zake na jamaa wa mume ndio watu wa kuwategemea kwa mwanamke aliyeolewa mbali na familia yake kwani hao ndio wenye dhamana naye kwa wakati wote atakapokuwa na mume huyo. Kipengele cha fani kilichoibuwa mafunzo hayo ni lugha, lugha ambayo ni nyepesi na ambayo inafahamika vizuri, ni Kiswahili sanifu, kwa mwongozo wa nadharia ya Simiotiki, neno nguzo ni ishara ya kitu madhubuti cha kutegemea.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, mafunzo hayo ni muhimu na mtu anayewapenda wakwe zake basi ndoa yake hudumu na hupendwa na wakwe zake, lakini mwanamke ambaye hawapendi wakwe zake na jamaa za mume wake, basi ndoa yake huwa na misukosuko kwani Waswahili husema, ukipenda boga upende na mti wake au mcha nyengine, ukipenda boga upende na ua lake. Kwahivyo, wimbo unatoa mafunzo kwa wanawake kuwapenda wakwe na jamaa wa mume kama anavyowapenda wazee wake na jamaa zake.

Katika utamaduni wa jamii ya Wapemba, suali la kutunza wakwe limepewa kipao mbele. Ni jambo maarufu sana kwani wakwe ni watu wanaoheshimika na kutunzwa vyema. Wapemba wanamsemo wao usemao, ómkwe kidondaö. Msemo huu huashiria umuhimu wa kutunza wakwe. Ni mfano wa mtu anavyokitunza kidonda chake kwa kuepuka kupata madhara zaidi. Na wanaamini bila ya wakwe zake asingalipata mume na usingizi mnono. Hivyo wakwe hupewa thamani, heshima na matunzo mazuri kwa lengo la kudumisha mapenzi kwa mume wake na kudumisha ndoa yake.

Nyimbo nyengine yenye kutoa mafunzo juu ya kuwapenda wakwe na jamaa wa mume ni*: "Ulivyotaka kuolewa wee, utampara samaki wee*ò

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, kipengele cha fani kilichoibua mafunzo hayo ni lugha ya ishara, samaki ni ishara ya mume, magamba, mkia, mapezi, miba ni ishara ya jamaa wa mume, kwani kama tunavyoelewa kuwa, magamba, mapezi, mkia, na miba ni sehemu za samaki kwa hivyo vimeashiria kuwa, mume naye ana wazazi wake na jamaa zake ambao anapaswa mke kuolewa kuwapenda na kuwathamini akielewa kuwa ni sehemu ya mume wake na bila ya wakwe basi asingalimpata mume huyo.

Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, kipengele cha fani tulichokieleza hapo juu, wimbo huu unatoa mafunzo kwa maharusi na kwa wanawake waliolewa kuwapenda na kuwatunza wakwe zake na kuwapenda jamaa wa mume, kama wimbo unavyosema: *"Ulivyotaka kuolewa we, utampara samaki",* ukiwa na maana mwanamke ametaka kuolewa na mume huyo, basi awapende na watu wake, ili kuzidisha mapenzi na mume wake na kudumisha ndoa yao.

Kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia, mafunzo haya husisitizwa sana kwa maharusi wa Kipemba, kwani wanaamini mke kuolewa hawezi kuishi na mume wake bila ya kumpendea wazazi wake na jamaa zake. Katika jamii tumeshashuhudia ndoa nyingi zikivunjika kutokana na wanawake kuolewa kuwadharau wakwe zao na jamaa za waume wao. Na pia kuna ndoa ambazo zimedumu kutokana na wanawake kuwapenda wakwe zao na jamaa za waume wao. Hivyo basi ni jukumu letu

wanawake walioolewa kuwapenda na kuwatunza wakwe zetu na jamaa za waume zetu ili ndoa zetu zidumu.

### 4.4.6 Mafunzo ya Kuwacha Tabia Mbaya

Mafunzo mengine yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo ni kutokuwa na tabia mbaya kama umbea na kurandaranda majiani na mitaani, pia tabia ya kugombana na kutukanana na majirani. Nyimbo zenye kutoa mafunzo hayo ni:

*"Mama ooo, watu wote waolewa, mie siolewi kwani"*

Kwa kuongozwa ni nadharia ya Uamilifu, wimbo huu unatoa mafunzo kwa maharusi kuwacha tabia mbaya ambazo hazikubaliki katika jamii, tabia mbaya hizo ni pamoja na, uchafu, kugombana na watu, kutukanana na majirani, kurandaranda ovyo mitaani. Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki kipengele cha fani kilichoibuwa mafunzo hayo ni lugha ya ishara, maneno kukojoa kitandani, chepu ni ishara ya uchafu, na kipengele chengine ni lugha nyepesi ambayo inafahamika wazi wazi.

Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, wanawake wenye tabia mbaya kama zilizotajwa katika wimbo huwa hawaolewi au hata wakiolewa kama hawakujirekebisha basi ndoa zao huwa hazidumu. Kwa jumla, wimbo unaeleza kwamba mtu akiwa na tabia mbaya si aglabu kuolewa, kwani watu humchukulia yuko kinyume na mila na desturi za jamii, tabia mbaya kama ya kutukana majirani ni aibu kubwa kwa jamii ya Wapemba, ni tabia inayochukiza mno na hupelekea mtu kukosa mume wa kumuoa.

Hii ni kutokana kuwa katika jamii ya Wapemba jirani ni mtu mwenye umuhimu wa pekee, majirani mara nyingi ndio wanaosaidiana kwa muda mrefu kuliko hata ndugu

na jamaa, kwa mfano mtu anapoumwa na kupata matatizo jirani ndiye mtu wa kwanza kumpa huduma hata jamaa na wazee wake hata wanapofika jirani tayari ameshamsaidia. Maswali haya ni miongoni mwa mila na desturi za Wapemba, hivyo wimbo unamfunza biharusi na wanawake wengine kuishi vizuri na majirani.

Wimbo unaendelea kueleza kuwa, pia ni tabia mbaya isiyokubalika kwa mwanamke mwenye kuolewa kurandaranda mitaani kama wimbo unavyosema: ñNa ila ya nne, kutwa kiguu njianiö

Katika jamii ya Wapemba, ni tabia mbaya isiyokubalika kwa mwanamke aliyeolewa kurandaranda ovyo mitaani bila ya ruhusa ya mume wake na bila ya sababu za msingi. Kwa kawaida mwanamke aliyeolewa anatakiwa abaki ndani kwake akifanya kazi za ndani na kumsubiri mume wake na kumpa huduma zinazostahiki. Lakini katika jamii za Wapemba leo hii wanawake wanarandaranda ovyo mitaani hajuilikani mwenye mume au asiyekuwa naye. Kwahivyo, wimbo unatoa mafunzo kwa maharusi wajiepushe na tabia hii mbaya.

Wimbo mwengine wenye kutoa mafunzo kama hayo ni: ñ*Hodi, hodi, hodi, wee*, *hodi ya mwana mirambo"*

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki lugha ya ishara imetumika katika kutoa mafunzo juu ya wimbo huu. Lugha ya ishara iliyotumika ni, hodi, hodi, hodi, hodi hizi zinashiria ni mgeni ameingia mtaani, hodi ya mwana mirambo yaani hodi ya mgeni mirambo ni ishara ya mgeni aliyeingia mtaani. Kwa mwongozo wa nadharia ya Uamilifu, wimbo unatoa mafunzo kwa maharusi na kwa wanawake walioolewa kujitahidi kuishi vizuri mitaani kwa watu, kwani kwa vyovyote vile yeye ni mgeni na

kama wasemavyo Waswahili, mgeni hachomi nguru akanuka, msemo huu una maana ya kuwa mtu akiwa ugenini, basi asifanye tabia mbaya ambazo zitawakera wenyeji wake. Wimbo unasisitiza kuwa mgeni havunji kiambo ikiwa na maana mgeni asiwe na tabia mbaya, ambazo zinakwenda kinyume na mila na desturi za jamii yake anayoishi. Kwa mwongozo wa nadharia ya Sosholojia, katika jamii ya Wapemba, watu wenye tabia mbaya mpaka wakawakera wenyeji wao, watu hawo huwa wagombanishaji wa watu, wenye kuchunguza mambo ya watu, huchukuwa waume wa wenziwao na wengine huwa wizi.

Kwahivyo, wimbo huu, una mtahadharisha bi harusi na wanawake wengine kuwacha tabia mbaya ambazo zinakwenda kinyume na jamii zetu. Wanawake wenye tabia mbaya aglabu hurudisha kwao yaani huachwa kabisa kutokana na tabia zao mbaya na wala hawawezi kujirekebisha. Wanawake tuwache tabia mbaya ili tuishi vizuri katika ndoa zetu na kujenga mapenzi kwa waume wetu na tudumishe ndoa zetu.

### 4.4.8 Mafunzo ya Kujenga Mashirikiano na Maelewano Katika Maisha ya Ndoa

Nyimbo za msondo pia zinatoa mafunzo ya kujenga maelewano na masikizano katika maisha ya ndoa. Nyimbo zenye kutoa mafunzo hayo ni: ñ*Saada kaolewa, muacheni aolewe, anenepe aote mkia"*. Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, wimbo umetumia lugha ya ishara katika kutoa mafunzo kwa jamii, neno besera ni ishara ya mali au utajiri au kitu cha thamani kubwa. Na neno óuaô ni ishara ya mwanamke. Aidha taswira imetumika, taswira wenyewe ni huko pwani kuna ua, lachanua kimanjano. Hii ina maana ya kuwa, mwanamke amependeza yuko tayari kwa kuolewa. Wimbo unaendelea kusema: ó*Ukitaka kulichuma, ulichumie sindano'*

Mshororo huu una maana ya kuwa óuaôukitaka kulichuma sharti ulichumie sindano. Maneno hayo yanaashiria kwamba, mwanamke anapotaka kuolewa kuna taratibu zake na masharti ambayo mwanamme anatakiwa ayafuate. Kwahivyo, wimbo unasema ókuolewa si besera, hoja ni masikizano. Kwa kuongozwa ni nadharia ya Uamilifu, ambayo inasisitiza kuwa, kazi yoyote ya fasihi ni lazima iwe na ujumbe kwa jamii, kutokana na vipengele vya fani vilivyovitaja, wimbo huu unatoa mafunzo kwa maharusi kuwa, kuolewa si besera hoja ni masikizano. Maana yake ni kuwa kuolewa sio kupata mali au utajiri au kitu cha thamani au mbanjo nyingi au vyombo vingi vya kuoneshana, bali kuolewa ni mafahamiano kati ya mume na mke wake, au mke na wakwe zake na majira zake. Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia, ambayo inasisitiza kazi ya fasihi ni iwe yenye kuakisi jamii, kwa hivyo wimbo huu umeakisi jamii, kwani katika jamii ya Wapemba, mwanamke hupewa mahari, lakini kuna baadhi ya familia wanafanya kama wanawake ni biashara, yaani wanadai mahari makubwa kiasi ambacho wanaume wanashindwa kuowa kutokana na mahari kuwa makubwa, na familia nyengine mahari yanakuwa ni ya kawaida, kinachoangaliwa ni kuwa mwanamume ni mtu mzuri, yaani ni mtu mwenye tabia nzuri. Jambo linalosisitizwa ni mafahamiano na masikizano kati ya mke na mume, kama wimbo unavyoeleza: *"Kuolewa si besera, hoja ni masikizano"* Hii ina maana kuolewa sio kupata utajiri bali ni kuwa na mafahamiano kati ya mke na mume.

## 4.4 Vipengele vya Fani vya Nyimbo, Jinsi Vinavyosaidia Kufikisha Mafunzo kwa Walengwa

Vipengele vya fani vya nyimbo vilivyosaidia kufikisha mafunzo kwa walengwa katika nyimbo zilizokusanywa ni pamoja na tamathali za semi kama vile sitiyari,

tauria, ishara, taswira. Vipengele vyengine ni pamoja na mafumbo, kejeli nakadhalika. Nyimbo zilizo na mafunzo juu ya ustahamilivu wa shida na matatizo katika maisha ya ndoa ni:

*'Raruwa ee dereva rarua wee"*

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, vipengele vya fani vilivyosaidia kuibua mafunzo kwa walengwa ni lugha ya ishara ambapo imeibua mafunzo ya ustahamilivu juu ya shida na matatizo yanayotokea katika maisha ya ndoa. Lugha ya ishara iliyotumika ni maneno, dereva ikiwa ni ishara ya mume au mke, mlima ni ishara ya maisha ya ndoa kwa ujumla, mawe, tope, utelezi hizo ni ishara ya shida na matatizo yanayoweza kutokea katika maisha ya ndoa. Kwa kutumia ishara hizo wimbo unatoa mafunzo kwa maharusi mke na mume yakuwa katika maisha ya ndoa kuna shida na matatizo ambayo yanaweza kutokea, kwa hivyo ni kwao maharusi kuwa wastahamilivu kwani ndoa wameikubali wenyewe na wamekubaliana wenyewe.

Wimbo mwengine wenye mafunzo kama hayo na vipengele vya fani vilivyoibua mafunzo hayo ni: ñ*Ushangia mapengomsumeno wangu wee".*

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, vipengele vya fani vya nyimbo vilivyosaidia kuibua mafunzo hayo ni tauria, lugha ya picha, sitiari. Neno msumeno ni tauria yenye maana ya mume, mapengo, haukerezi ni ishara ya kuwa, mume hana nguvu za kujamii, mama nataka karanga, hii ni tauria yenye maana ya kuwa, mke anataka haki ya ndoa, lakini msumeno umeshangia mapengo haukerezi. ñKaukarange chini ya gaeò hii ni taswira yenye kuibua mafunzo ya kuwa kama kumetokea matatizo ya

mume kukosa nguvu basi mwanamke atafute dawa, dawa ya kwanza ni kufanya matayarisho ya hali ya juu ikiwa ni pamoja na kujipamba vizuri, kufukiza udi na kutumia manukato ya aina kwa aina, na pia kumkanda, kumchezeachezea mume wake katika sehemu zenye kuleta hisia, na kama hakuna mafanikio basi nikutafuta dawa za kienyeji au kutafuta ushauri kwa waganga wa kienyeji au wa hospital kwani huenda tatizo likawa sio kubwa.

Kwahivyo, kwa kupitia vipengele hivyo vya fani wimbo huo unatoa mafunzo kwa maharusi kuwa wastahamilivu wanapokutana na matatizo kama hayo, wawe wastahamilivu huku wakitafuta dawa na ushauri kwa wataalamu wa tiba na wala sio kumkimbia mume, kama wimbo unavyosema: ñkama haukerezi nitakwenda zangu mieò

Kwenye nyimbo zenye mafunzo ya kumuenzi na kumuheshimu mume, vipengele vya fani vilivyosaidia kuibua mafunzo hayo ni lugha ya kawaida inayofahamika kwa wepesi, mfano wimbo wa sanyombe sanyombe mwari wangu wee unavyosema: *“Sanyombe sanyombe mwanangu wee”.* Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, wimbo unaonekana kutumia lugha nyepesi ya kawaida, kwahivyo mafunzo yako wazi wazi.

Katika nyimbo zenye mafunzo ya kumtunza na kumdhibiti mume vipengele vya fani vilivyosaidia kuibua mafunzo hayo ni lugha ya ishara, lugha ya picha, sitiyari. Kwa mfano katika wimbo huu: ñ*Viti viwili mfano, matendegu sawasawa”*

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki ambayo inaangalia ishara zilizotumika katika kazi ya fasihi zina rejelea nini, katika wimbo huu kuna matumizi ya tamathali za usemi ya sitiari, ishara, taswira, tauria na tashibiha.

Viti viwili matendegu sawasawa, hizi ni ishara ya bibi na bwana harusi wanaolingana sawasawa, pia ni sitiyari inayohusisha matendegu na hao wapendanao. Neno ufunguo ni ishara ya matunzo na kumdhibiti mume, kwahivyo wimbo unatoa mafunzo kwa wanawake wenye waume wawape matunzo mazuri waume, kwani kama hapana matunzo mume atachukuliwa na wenye mapenzi na wenye matunzo na udhibiti wa waume, kama wimbo unavyosema: óAkiacha ufunguo, watachukua wenzioô

Wimbo mwengine ni: ó*Ndege huyo, nzuri kwa maua,*

*Hata akipata uchanja, ndege atatua'*

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, vipengele vya fani vilivyosaidia kutoa mafunzo kwa walengwa katika wimbo huu ni ishara na taswira na mafunzo wenyewe ni juu ya kumtunza na kumdhibiti mume. Neno óndegeô linaashiria mume na ómauaô ni ishara ya mke, ishara hizo zinamaanisha kuwa, mume hupendeza anapoenziwa, anapotunzwa na kudhibitiwa na mke wake, kwahivyo mke ni wajibu wake kumtunza mume wake. Neno óuchanjaô ni ishara ya matunzo, hivyo mwanake akishindwa kumtunza na kumdhibiti mume, mume huyo huenda akatafuta mwanamke mwengine akitarajia kupata matunzo mazuri, kama wimbo unavyosema: óHata akipata uchanja, ndege atatua hii pia ni taswira.

Mfano wa nyimbo zenye mafunzo ya kutunza siri za maisha ya ndoa, na vipengele vya fani vilivyosaidia kufikisha mafunzo kwa walengwa ni: *'Mwari wangu wenda kwako, kuna mambongwa ukoo".* Kwa mwongozo wa nadharia ya Simiotiki, vipengele vya fani vilivyosaidia kufikisha mafunzo kwa walengwa ni ishara, taswira

na hata tauria. Maneno ókijunguô, kitanda, mirimo, mabonde, mashimo ni lugha za ishara. Kijungu ni ishara za siri zinazopatikana jikoni, ikiwa na maana ya kuwa mwanamke anatakiwa atunze siri za jikoni kwake asijuilikane na watu leo amepika nini au leo amekula nini? Pia asihadithie kwa watu leo nimepika nini, neno kitanda ni ishara ya siri za kitandani kati ya mke na mume wake, ikiwa na maana mwanamke anatakiwa asiwe mwenye kutoa siri za kitanda, mwanamke anatakiwa asihadithie mambo wanayofanyiana na mume wake, ikiwa ni sehemu ya mapenzi ya ndoa yao.

Neno mirimo mabondeô na ómashimoô ni taswira zinazoonesha katika maisha ya ndoa kuna raha, shida na matatizo, yote hayo mtu anatakiwa awe nayo moyoni, na wala asitangaze hadharani kama ni raha au shida. Kwenye nyimbo zenye mafunzo ya kujiepusha na wanaume wa nje, vipengele vya fani vilivyosaidia kufikisha mafunzo kwa walengwa ni kama vile ishara, taswira na sitiyari.
Mfano wimbo huu: ñ*Kuna videge viwili mwanangu, vitakuja na tishio"*

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, maneno óvidege viwiliô ni ishara ya wanaume wenye macho ya nje, neno ótishioô ni tauria yenye kuficha makali, tishio hapa ni watamtongoza yaani wanaume watamtongoza, kwahivyo wimbo, unatoa tahadhari kwa maharusi na wanawake wengine kuwa, waachane na wanaume wa nje ya ndoa yao, kwani raha ya ndoa ni kustarehe na mume wako.

Wimbo mwengine ni: *Maroma hayana ukweli".* Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, maneno ómaromaô ni ishara ya wanaume wa nje, na neno babindoô ni ishara ya mume wa ndoa, neno chengere chengere ni tauri yenye maana ya kutongozwa au kushawishiwa. Kwa jumla, kutokana vipengele hivyo wimbo unatoa mafunzo kwa

maharusi wa kike na wanawake wengine, kuwa wanaume wa nje hata wakikutongoza usiwakubalie kwani hawana ukweli ni watu hadaa na wala hawana mapenzi ya kweli wanataka kumkashifu mtu tu baadae wamuache papo, ni vizuri wanawake kuishi vizuri na kwa mapenzi na waume wao.

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, katika wimbo huu kumetumika tamathali za usemi za tauria, sitiari, ishara na taswira. Tamathali ya usemi ya tauria ni kuwa wimbo umeficha siri ya matusi na maneno ya karaha, lakini hapa tutaifichuwa kidogo ni kwamba kisiki ni mume ambaye yuko tayari anataka starehe baada ya matayarisho mazuri ya mke wake. Tamthali ya usemi ya tashhisi pia imetumika ni kisiki kupewa uhai, kinachezacheza na kumwaga mchanga, yaani mume tayari ameshasimama na kuonesha hamu ya kula. Na tamathali ya usemi ya ishara imetumika kwamfano, kisiki ni ishara ya mume, na waganga ni ishara ya mke, yaani mume anataka starehe basi mkewe amgange. Na taswira iliyotumika ni kaukarange chini ya gae.

Kwa ujumla, vipengele vya fani vilivyosaidia kufikisha ujumbe kwa walengwa ni tamthali za usemi kama vile sitiari, tauria, ishara, tashhisi, mafumbo na hata kejeli zimetumika katika nyimbo hizi za ngoma ya msondo.

# SURA YA TANO

# HITIMISHI, MUHTSARI NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ameelezea hitimishi, muhtasari wa utafiti na mapendekezo yaliyopendekezwa katika tasnifu hii.

## 5.2 Hitimishi

Utafiti huu unahusu, kuchunguza dhima za nyimbo za ngoma ya msondo. Madhumuni mahsusi ni kuzikusanya nyimbo hizo za ngoma ya msondo, kuanisha dhima zinazopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo, kuanisha mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo na mwisho ni kujadili vipengele vya fani, jinsi vilivyosaidia kufikisha mafunzo kwa walengwa. Utafiti huu una sura tano, sura ya kwanza inahusu Utangulizi kwa ujumla, sura ya pili inahusu Utalii wa kazi tangulizi na Mkabala wa Kinadharia, sura ya tatu inahusu Mbinu na njia ya utafiti, sura ya nne inahusu Uwasilishaji na Uchambuzi wa data, na sura ya tano inahusu Hitimishi na Mapendekezo. Mtafiti ametumia mbinu mbili kuu za kukusanyia data ambazo ni mbinu ya Maktabani na mbinu ya Usaili baina ya Mtafiti na Watafitiwa. Data za utafiti zilichambuliwa kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, nadharia ya Uamilifu, na nadharia ya Sosholojia.

Na mwisho kuchambua dhima na mafunzo katika kazi ya fasihi, sio jambo rahisi, kwani kwa kawaida kazi ya fasihi huwa ni fumbo ambalo halina jawabu moja. Kwahivyo, mtafiti mwengine akizisoma nyimbo hizi, anaweza kugunduwa mafunzo mengine ambayo mtafiti hakuyagusia au kuyafafanua kulingana na ufahamu wake na

nadharia zilizomwongoza. Kwahivyo, mtafiti mwengine anaweza kuanzia hapa mtafiti wa kazi hii alipofikia. Aidha, tasnifu hii ilihusu kuchunguza dhima na mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za msondo wa Wapemba katika shehia ya Kengeja, Mwambe na Mkungu, kwahivyo, mtafiti mwengine yuko huru kufanya utafiti katika shehia nyengine na akachunguza na kuzikusanya nyimbo hizo zaidi au hata kuchunguza sababu hasa zilizosababisha nyimbo za ngoma ya msondo kuwachwa, wakati ilikuwa ni taasisi madhubuti ya kufunzia maharusi na jamii kwa jumla.

## 5.3 Muhtasari wa Utafiti

### 5.3.1 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu ni kwamba, mtafiti amegundua kuwa, nyimbo za ngoma ya msondo zinadhima kubwa katika jamii, kwani zinawajenga wanajamii kuyamudu maisha yao (hasahasa maisha ya mdoa). Dhima zilizogunduliwa ni dhima ya kuelimisha kama ilivyo kazi ya fasihi, dhima hizo ni dhima ya kuelimisha wanawake kuwa wastahamilivu, wajege tabia ya usafi wa mwili na wa nguo, waishi vizuri na wakwe na jamaa wa mume, kushirikiana na mume wake na kuwa na maelewano mazuri. Dhima nyengine ni ile ya kuonya kutokana na tabia mbaya au watu wabaya ambao wanaweza kuhatarisha ndoa zao, na pia nyimbo za ngoma ya msondo zimeonekana nyengine ni zenye kutoa burudani kwa maharusi.

Mafunzo yaliyopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo ni pamoja na mafunzo ya ustahamilivu wa shida na matatizo katika maisha ya ndoa, mafunzo ya kumuheshimu na kumuenzi mume, mafunzo ya kumtunza na kumdhibiti mume au

mke, mafunzo juu ya utunzaji wa siri katika maisha ya ndoa, mafunzo ya kujiepusha na vishawishi vya wanaume wa nje ya ndoa, mafunzo juu ya kutunza usafi wa mwili na kujenga tabia ya kujipamba, mafunzo ya kuwapenda na kuwathamini wakwe na jamaa wa mume, mafunzo ya kuwacha tabia mbaya, mafunzo ya kujenga mashirikiano na maelewano kati ya mume na mke. Ufafanuzi zaidi unaonekana katika sura ya nne kwenye uchambuzi wa mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za ngoma ya msondo.

Vipengele vya fani vilivyosaidia kufikisha mafunzo kwa walengwa ni pamoja na mafumbo, tamathali za usemi kama vile sitiyari, tauria, ishara, taswira na kejeli, vipengele hivi vinaonekana katika sura ya nne kwenye uchambuzi wa vipengele hivyo pamoja na mifano yake.

Kwa jumla, nyimbo za ngoma ya msondo zinaonekana ni zenye kutoa elimu kubwa na pia zinatoa mafunzo kwa maharusi na wanawake wengine wenye waume na wanaotarajia kuolewa. Watafitiwa wengi walisisitiza kuwa, nyimbo za ngoma ya msondo zinastahili kuendelezwa na kudumishwa na kutumiwa katika shughuli zetu za harusi ili kurithisha kizazi chetu mila na desturi zetu na kuacha kabisa mila na desturi zisizokuwa zetu.

Mtafiti amegundua kuwa, nyimbo za ngoma ya msondo zinapotea na kusahaulika, mtafiti ameligundua hili wakati alipokuwa akiwahoji watafitiwa, watafitiwa wengine walijibu mwanangu we, nyimbo hizi ninazikumbuka tena, hebu nenda kwa fulani, na watafitiwa wengine walimjibu mtafiti, mimi sizikumbuki tena hebu njoo kesho au siku fulani.

## 5.4 Mapendekezo ya Utafiti

5.4.1 Kwa jamii zetu Wazanzibari, tuzienzi na kuzitukuza nyimbo za ngoma ya msondo kwani zinatumia lugha ya kifasihi iliyojaa mafumbo na kusheheni lugha ya kitamathali za usemi na kuibua mafunzo mazito kwa maharusi na wanawake wengine.

5.4.2 Kwa wazee wenye watoto wajitahidi kadri ya uwezo wao kuwafunza watoto mila na desturi za Kizanzibari ili waachane kabisa kufuata na kuzipenda mila na desturi za kigeni ambazo zinakwenda kinyume na mila na dasturi zetu. Aidha, tujitahidi kutumia nyimbo hizi za msondo katika shughuli zetu ili tuwape watoto mafunzo yatakayowawezesha kujua haki na wajibu wao katika maisha ya ndoa.

5.4.3 Kwa maharusi nao, ni jukumu lao kuyatumia mafunzo wanayopewa siku za harusi, ili kudumisha mapenzi katika ndoa zao na kuepuka kabisa talaka zisizo na misingi wala sababu za kisheria.

5.4.4 Kwa watafiti, wasomi wanaotegemewa na Taifa, ni jukumu lao kufanya utafiti zaidi juu ya tanzu tofauti za fasihi, ili kuzidi kufichuwa maarifa yaliyofumbatwa kwenye fasihi hiyo. Aidha, watafiti wajenge tabia na moyo wa uzalendo kwa kuzichapisha na kuzisambaza kazi zao kwa manufaa ya jamii, na watafiti wengine. Aidha, utafiti juu ya sababu zilizopelekea ngoma hii ya msondo kutoweka katika jamii zetu hata siku za harusi za watoto wetu.

5.4.5 Kwa Serikali zetu, zijuwe ni jukumu lao kusimamia kuenziwa mila na dasturi zetu na kuhifadhiwa na wajitahidi kupinga kwa vitendo, mila na dasturi ambazo ziko

kinyume na mila zetu, ambazo zinachangia kupotosha vijana wetu ambao ndio nguvu kazi ya Serikal zetu. Pia serikali ianzishe kwa makusudi ofisi za kuhifadhi ripoti za utafiti zinazofanywa na wasomi wetu, ili kuwasaidia wanafunzi kupata marejeleo katika masomo yao na pia kuangaliwa mapendekezo yanayotolewa na watafiti tofauti.

Na mwisho kuchambua dhima na mafunzo katika kazi ya fasihi, sio jambo rahisi, kwani kwa kawaida kazi ya fasihi huwa ni fumbo ambalo halina jawabu moja. Kwahivyo, mtafiti mwengine akizisoma nyimbo hizi, anaweza kugunduwa mafunzo mengine ambayo mtafiti hakuyagusia au kuyafafanua kulingana na ufahamu wake na nadharia zilizomwongoza. Kwahivyo, mtafiti mwengine anaweza kuanzia hapa mtafiti wa kazi hii alipofikia. Aidha, tasnifu hii ilihusu kuchunguza dhima na mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za msondo wa Wapemba katika shehia ya Kengeja, Mwambe na Mkungu, kwahivyo, mtafiti mwengine yuko huru kufanya utafiti katika shehia nyengine na akachunguza na kuzikusanya nyimbo hizo zaidi au hata kuchunguza sababu hasa zilizosababisha nyimbo za ngoma ya msondo kuwachwa, wakati ilikuwa ni taasisi madhubuti ya kufunzia maharusi na jamii kwa jumla.

## 5.5 Hitimisho

Utafiti huu unahusu kuchunguza dhima za nyimbo za ngoma ya msondo. Matokeo ya utafiti huu ni kwamba nyimbo za ngoma ya msondo wa Pemba kama zilivyokazi za fasihi zina dhima ya kuelimisha wanandoa namna ya kuishi katika maisha ya ndoa na kuepuka kabisa mambo au vitendo vinavyopelekea kuvunjika kwa ndoa. Mafunzo yanayopatikana ni pamoja na kuwa wastahamilivu kutokana na shida na matatizo

yanayotokea katika maisha ya ndoa, kuenziana kati ya mke na mume katika ndoa yao, kuwapenda wakwe kwa mke na mume, kuepuka tabia mbaya kama vile umbeya, uchafu, upekepeke, kutunza siri za maisha ya ndoa, kuheshimiana na kuthaminiana kati ya mke na mume. Na mwisho mtafiti katoa mapendekezo kwa serikali, kwa jamii, kwa wazazi na walezi na kwa maharusi.

## MAREJELEO


Ali, H. (2005). Mafunzo Yanayopatikana Katika Nyimbo za Harusi Katika Ndowa za Unguja, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Ali, Z. (2005). Athari za Nyimbo za kale za harusi katika ndoa za Wazanzibari, Chuo Kikuu cha Taifa.(Haijajapishwa).

Baraza la Kiswahili Zanzibar, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, Oxford University Press, Nairobi.

Bakar, K. (2008). *Utamaduni wa Wazanzibari*, Zanzibar Tanzania, Ouark Press Printing Servies.

Bulane, M. (1981). Fasihi Simulizi katika Afrika ya Kusini, Fasihi Simulizi ya Wenyeji katika Makala ya Semina za Fasihi Simulizi, Dar-es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Campbell, C. (1976), *An Introduction to the Music of Swahili Woman*, Institute of Africa Studies, Chuo Kikuu Nairobi.

Coppens, F. (1980), Wedding Customs in Lamu Society. (Haijachapishwa).

Enon, J. (1998). *Educational Research Statistics and Measurement*, Makerere University, Uganda.

Farsy, A. (1956), *Ada za Harusi katika Unguja*, East Africa Literature Bereau Nairobi.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*, Oxford University Press, Nairobi

Finnegan, R. (1977). *Oral Literature in Africa*, Oxford University Press, London.

Finnegan, R. (1994). *Oral Literature in Africa*, Oxford University Press, Nairobi.

Kavugha, F. A (1977). *Dasturi na Mila za Wapare*, Vuga Press, Soni.

Kirumbi, P. (1979). *Misingi ya Fasihi Simulizi,* Shugwaya Publishers Ltd, Nairobi.

Kipury, N. (2002), *Oral Literature of the Masai,* East Afica Publishers Ltd, Nairobi.

Kingei, K. (1997). Fasihi, Kioo cha Lugha, Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar es Salaamu, Dar es Salamu

Kingei, K. (2001). Nafasi ya nyimbo za Kiswahili za Taraab katika jamii ya Kisasa, Katika Kioo cha Lugha, Idara ya Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaamu.

Kothari, R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi, India.

Kothari, R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques,* New Age International Ltd, New Delhi.

Lunenburg, F. (2008). Writing a Successful Thesis or Dissertation, Crown Press A SAGE Company, USA.

Matteru, M. (1987). Tanzu za Fani na Fasihi katika Mulika 19, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaamu.

Mbarouk, J. (1981). Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Watoto, Tasnifu (M.A Kiswahili) ya Chuo Kikuu cha Taifa, Zanzibar.

Mdungi, A. (2010). Nafasi ya Mafumbo katika Nyimbo za Harusi, Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha ST.CLEMENTS, Zanzibar.

Msokile, M. (1981). Nafasi za Nyimbo za Fasihi Simulizi katika jamii inayobadilika, Makala ya Semina ya Fasihi Simulizi, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Msokile, M. (1991). *Miongozo ya Lugha na Fasihi*, Dar es Salaam University Press, Dares Salaam.

Msokile, M. (1993). *Uchambuzi na Uhakiki*, Dar es Salaamu University Press, Dar es Salaamu.

Mulokozi, M. (1983). Utafiti wa Fasihi Simulizi, katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili111, Fasihi, Taasisi ya Uchunuzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili,* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Muhammed, O. (2009). Mchango wa Nyimbo za Unyago katika kumkomaza mwari kiunyumba, Tasnifu ya M. A Kiswahili (Haijachapishwa).

Muhammed, M. na Muhammed, S (2002). *Kamusi ya Visawe,* English Press Ltd, Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu,* Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Njogu, K na Wafula, R. (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi*, The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Nyenyembe, S. (1996). *Kuwaandaa Watahiniwa wa Kiswahili*, Taasisi ya Elimu Tanzania.

Ndungu, M. na Wafula, R. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*, University of Nairobi.

Omar, S. (2008). *Fasihi Simulizi na Jinsia,* Mifano kutoka nyimbo za watoto Tanzania katika Kiswahili, Taasis ya Uchunguzi Kiswahili, Dar es Salaam.

Omar, S. (2012). Mulika No, 31, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Panneerselvan, R. (2004). *Research Methodology*, PHI Learning Private Limitted, New Delhi.

Rashid, H. (2013). Mafunzo ya Nyimbo za Jando na Unyago kwa jamii ya Wahiyao, Tasnifu ya M.A Kiswahili Fasihi ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Ruhumbika, G. (1983). Tafsiri za Fasihi za Kigeni katika ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili, katika Makala ya Semina ya Kitaifa ya Waandishi wa Kiswahili 111, TUKI, Dar es Salaam.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*, AERA Kiswahili Research Products, Dar es Salaam.

Sengo, T. (1985). Ph D: Folktales from Pemba and Unguja, University of Khartoum, Khartoum.

Senkoro, F. (1982). *Fasihi*, Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

Senkoro, F. (1987). *Fasihi na Jamii*, Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

Seif, D. (2011). Nyimbo za Jando na Unyago katika jamii ya Kikaguru, Tasnifu ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Oxford University Press, Nairobi.

TUKI (2006), *English Swahili Dictionary*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele vyake*, Phoenix Publishers Ltd, Nairobi.

Wamitila, K. (2003). *Kichoheo cha Fasihi Simulizi na Andishi,* Focus Publisher Ltd, Mombasa.

Wamitila K. (2008). *Kazi za Fasihi, Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi,* Phoenix Publishers Ltd, Nairobi.

# VIAMBATANISHI

## Kiambatanishi Na. I: Maswali ya Mahojiano Yaliyotumika Katika Kukusanya Data

1. Jina lako nani?
2. Una miaka mingapi?
3. Unaishi wapi?
4. Jinsi
5. Je, umeowa/umeolewa
6. Je, unaifahamu ngoma ya msondo?
7. Je, ngoma ya msondo hupigwa wakati gani?
8. Je, inapopigwa ngoma hii huwa kuna lengo lolote?
9. Je, ulipoowa/ulipoolewa ulipigiwa ngoma ya msondo?
10. Je, nyimbo za ngoma ya msondo zilikusaidia vipi katika maisha yako ya ndowa?
11. Je, unaweza kuniimbia nyimbo za ngoma ya msondo kama mbili au tatu?
12. Je, unaweza kuniambia dhima/kazi za nyimbo hizi kwa maharusi?
13. Hebu nieleze mafunzo wanayoyapata maharusi katika nyimbo hizi ulizoniimbia
14. Je, kwa hisia zako nyimbo za ngoma ya msondo zinapoimbwa siku hizo za harusi huwasaidia maharusi katika maisha yao ya ndoa?
15. Kwa mtazamo wako kuna tafauti kati ya maisha ya maharusi wanaopigiwa ngoma hii ya msondo na wale wasiopigiwa?

16. Unaweza kunieleza kwanini maharusi wetu wa zama hizi hawapigiwi ngoma ya msondo.
17. Una maoni gani juu ya ngoma ya msondo?

**Kiambatanishi Na. II: Nyimbo za Ngoma ya Msondo Zilizotumika Katika Utafiti**

**Nyimbo Zenye Mafunzo ya Ustahamilivu ya Shida ya Matatizo**

***Ushangia mapengo msumeno wangu***

*Ushangia mapengo msumeno wangu wee*

*Kama haukerezi nitakwenda zangu wee*

*Mama nataka karanga wee, kaukarange na ule mdude*

*Kama hauna mafuta wee, kaukarange kwa maji ya kunde*

*Nikaukarange wapiwee, kaukarange chini ya gae.*

***Raruwa dereva rarua***

*Raruwa dereva raruwa wee, raruwa dereva raruwa wee*

*Ulivyotaka kwa hiyari yako utaupanda mlima*

*Mlima una mawe huo, utaupanda mlima*

*Mlima una tope huo, utaupanda mlima*

*Mlima wateleza huo, utaupanda mlima.*

**Nyimbo Zenye Mafunzo Ya Kumuheshimu Na Kumuenzi Mume**

***Jina la wimbo: Sayombe sayombe mwari wangu***

*Sanyombe sanyombe mwanangu wee*

*Sanyombe mwanangu wee*

*Mume aitwa bwana mwari wangu wee*

*Mume atandikiwa, mwari wangu wee*

*Mume anapokewa, mwari wangu wee*

*Mume anaagwa, mwari wangu wee.*

*Jina la wimbo:* ***Yuwapi bibie harusi***

*Yuwapi wee yuwapi mamae harusi aje hapa tuhangaike naye*

*Mama yake harusi, twamtaka aje hapa*

*Shangazi yake harusi, twamtaka aje hapa*

*Na bibi yake harusi, twamtaka aje hapa*

*Na somo yake harusi, twamtaka aje hapa*

*Tuje tumfunze mwari asende kufedheheka*

*Ukiitwa na mumeo mama wajibu kumuitika*

*Ukiitwa ewe bibi uitikie bwana labeka*

*Umridhie mumeo mama kwa kila analotaka*

*Ati aje hapa tuhangaike naye, aje hapa tuhangaike naye.*

**Mafunzo ya Kumuenzi na Kumdhibiti Mume**

*Jina la wimbo:* ***Ndege huyoo***

*Ndege huyo mzuri kwa maua*

*Hata akipata uchanja ndege atatua*

Jina la wimbo: ***Ukitaka mume akae***

Ukitaka mume akae, kutandika kuna maanaye

Ukitaka mume aishi, kutandika kuna maandishi

Ukitaka mume adumu, kutandika kuna maalumu

Ukitaka mume apende, umrambe kama peremende

Viti viwili mfano, matendegu sawasawa

Ooo matendegu sawasawa, ooo matendegu sawasawa

Kungwi mfunze mwario, asiache ufunguo

Akiacha ufunguo, watachukua wenzio

**Nyimbo Zenye Mafunzo ya Kutunza Siri za Ndoa**

*Jina la wimbo:* ***Kakae mama kakae***

*Kakae mama kakae*

*Ukakae na mume*

*Siri za nyumba ni mbili*

*Mama kupata au kukosa*

*Jina la wimbo:* ***Mwari wangu wenda kwako***

*Mwari wangu wenda kwako, kuna mambongwa uko*

*Usikute kijungu ufunue, kuna mambongwa uko*

*Mwanangu wenda kwako, kuna mambongwa uko*

*Usikute kitanda utandue, kuna mambongwa uko*

*Usikute mambongwa ukasema, kuna mambongwa uko*

*Kuna mirimo mirimo mabonde na mashimo, kuna mambongwa uko*

**Nyimbo Zenye Mafunzo ya Kudumisha Usafi, Kujipamba na Kujirembaremba**

*Jina la wimbo:* ***Jiwe jiwe limpambwa***

*Jiwe, jiwe, jiwe limpambwa wee*

*Limetiwa herini na wanja, jiwe limbambwa wee*

*Nekuwa na gamu ya mume wa mwanangu*

*Hejiokotea machakacha, leo kampata mchuchu wa haja wee*

*Jina la wimbo:* ***Mwari aingizwe chooni***

*Mwari aingizwe chooni, kwa maulidi*

*Tukampake marashi uvumba na udi*

*Oooo uvumba na udi wee*

*Uvumba na udi wee*

**Nyimbo Zenye Mafunzo ya Kujiepusha na Wanaume wa Nje**

Jina la wimbo: ***Mmaliwa mmaliwa***

Mmaliwa mmaliwa, mmaliwa mmaliwa,

Mwenzenu kashaolewa leo aja chukuliwa

Huko pwani kuna mti, waitwa mgome gome

Ukitaka kuuchanga, ukae chini usome

Wanaume wa wenzio, kuwachukua ukome

***Jina la wimbo: Videge viwili***

Kuna videge viwili mwanangu, vitakuja na tishio

Vitakufata fata mwanangu, kwa njia ya matamanio

Jua raha ya mapenzi mwanangu, ni kulala na mumeo

Jina la wimbo: ***Maroma***

Maroma hayana ukweli, ukisikia chengere chengere

Funguo za baskeli, maroma yana hadaa

Kama si babindo wangu ndani, ningali lala na njaa

**Nyimbo Zenye Mafunzo ya Kuwapenda na Kuwathamini Wakwe na Jamaa Wa Mume**

Jina la wimbo: ***Mwana wapende wakwezo***

***Mwana*** wapende wakwezo, we mtoto hoya

Hizo kwako ndio nguzo, we mtoto hoya

Ujapopata tatizo, we mtoto hoya

Nikimbilio la mwanzo, we mtoto hoya

Jina la wimbo: ***Ulivyotaka kuolewa***

***Ulivyotaka*** lewkuolewa we, utampara samaki we

Samaki ana magamba we, utampara samaki we

Samaki ana vumba we, utampara samaki we

Samaki ana miba we, utampara samaki we

Bwa mjuma we bwa mjuma ana mliowe akuruza

**Nyimbo Zenye Mafunzo ya Kuwacha Tabia Mbaya**

Jina la wimbo: ***Ila***

Una ila moja ila yako wewe ila hutaki kupika ila

Una ila moja ila yako wewe ila ukisemeshwa husemi ila

Una ila moja ila yako wewe ila kusema nimechoka ila

Jina la wimbo: Bi Yaya

Bi Yaya ooooo bi Yaya

Watu wote waolewa mie siolewi kwani

Una ila ila moja wakojowa kitandani

Na ila ya pili, watukana majirani

Na ila ya tatu, wagombana na wahisani

Na ila ya nne, kutwa kiguu njiani

Kanijengee kibanda kwetu Tundauwa

Washanigeuza mwendo chepu wataniuwa

Jina la wimbo: ***Nyonyo***

Nyonyo wee nyonyo wee kanipeleke nikanyony

Kisima cha Mangapwani kina majani majani nyonyo

Ukitaka kunywa maji uwe na mdu kwapani nyonyo

Kisima kihali hii wenyewe wa hali gani nyonyo